# KUCHUNGUZA DHIMA YA METHALI ZA JAMII YA WASIMBITI WA RORYA MKOANI MARA

**ANGELA GHATI SYLVESTER**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2016**

## UTHIBITISHI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo ***Kuchunguza Dhima ya Methali za Jamii ya Wasimbiti wa Rorya Mkoani Mara,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

…………………………………………..

**Sheikh, Profesa, Daktari, T.S.Y.M. SENGO**

**(Msimamizi)**

…………………………………………..

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

# TAMKO

Mimi, **Angela Ghati Sylvester**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

………………………………

Saini

………………………………

Tarehe

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa familiya yangu akiwemo mume wangu Sixbert Mwesiga na watoto wangu Philomena na Specioza. Pia natabaruku kazi hii kwa jamii ya Wasimbiti wote wa Wilayani Rorya.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na subira katika kipindi chote cha masomo yangu tangu wakati wa masomo ya darasani na kisha utafiti. Napenda kutoa shukurani zangu zisizo kifani kwa msimamizi wangu Prof. T.S.Y.M. Sengo kwa kujitoa katika kunielekeza, kunifundisha, kunikosoa na kunitia moyo wa kuongeza juhudi katika masomo. Vilevile, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa walimu wote walionifundisha masomo ya shahada ya uzamili na kuniwezesha kufika katika hatua hii. Walimu hao ni Prof. Emmanuel Mbogo, Dkt. P. P. Lipembe, Dkt. Elisifa Zelda, Dkt. Hanna Simpassa na Dkt. Mohamed Omary. Nawashukuru sana walimu wangu kwa kunivusha katika jahazi la wasafiri wa shahada ya uzamili katika Kiswahili. Pia napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu kwa kuniwezesha kusoma kwa utulivu katika kipindi chote mpaka kufikia hatua hii. Namshukuru mume wangu bwana Sixbert Mwesiga kwa kunigharamia masomo yangu na pia kunipatia ruhusa ya kusoma shahada ya uzamili katika Kiswahili. Pia, nawashukuru watoto wangu, Philomena na Specioza kwa kuwa wavumilivu kwa kunikosa nyumbani mara kwa mara nikiwa masomoni. Nasema asanteni sana. Vile vile nawashukuru wazazi wangu Mzee Sylvester Kenemo na Mama Viktori Kenemo kwa kunishauri na kunipa moyo wa kufanya utafiti huu na walikuwa chachu yakunipatia methali ambazo nazo zimetumika katika utafiti huu. Pia nawashukuru wazee wote wa jamii ya Wasimbiti, wanafunzi wa Kidato cha Tatu 2015 Shule ya Sekondari Waningo na uongozi wote kwa ujumla ambao walikuwa bega kwa bega kunipa msaada wa kupata methali za jamii hiyo na hatimaye kukamilisha utafiti huu.

## IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza dhima ya methali za jamii ya Wasimbiti wa Rorya mkoani Mara. Ili kufanikisha mada hii utafiti ulikuwa na madhumuni mahususi matatu ambayo ni kubainisha dhima ya methali ya jamii ya Wasimbiti wa wilaya ya Rorya mkoani Mara, kuelezea uhalisia wa dhima za methali za jamii ya Wasimbiti kwa jamii ya leo na kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika kujenga dhima za methali za jamii ya Wasimbiti. Madhumuni haya matatu yamefanyiwa kazi na matokeo ya utafiti yamepatikana. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili na upitiaji wa nyaraka na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia za Sosholojia na Simiotiki. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa methali za jamii ya Wasimbiti zina dhima za kuhamasisha jamii kuepuka tamaa , kuwa na subira, kuelimisha jamii juu ya maisha, kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, kuhimiza umoja na mshikamano katika jamii na umuhimu wa malezi kwa vijana katika jamii. Pia, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa methali za jamii ya Wasimbiti zinaundwa na mbinu za kisanaa za mafumbo, takriri, taswira na muundo. Mbinu hizi za kisanaa zimesaidia sana katika kuwasilisha dhima za methali za jamii ya Wasimbiti wanaoishi wilaya ya Rorya mkoani Mara.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHI** ............ **ii**

**HAKIMILIKI** ............ **iii**

**TAMKO** ............ **iv**

**TABARUKU** ............ **v**

**SHUKURANI** ............ **vi**

**IKISIRI** ............ **vii**

**YALIYOMO** ............ **viii**

**SURA YA KWANZA** ............ **1**

**1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI** ............ **1**

1.1 Utangulizi ............ 1

1.2 Historia Fupi ya Jamii ya Wasimbiti na Methali Zao ............ 1

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti ............ 4

1.4 Tatizo la Utafiti ............ 6

1.5 Malengo ya Utafiti ............ 7

1.4.1 Lengo Kuu ............ 7

1.4.2 Malengo Mahususi ............ 7

1.4.3 Maswali ya Utafiti ............ 8

1.5 Umuhimu wa Utafiti ............ 8

1.6 Mipaka ya Utafiti ............ 9

1.7 Mpangilio wa Tasinifu ............ 9

**SURA YA PILI** ............ **10**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** ............ **10**

2.1 Utangulizi .......... 10

2.2 Utafiti wa Methali Duniani .......... 10

2.3 Mbinu za Kisanaa katika Methali .......... 15

2.4 Kazi Tangulizi za Methali za Kitanzania .......... 20

2.5 Mkabala wa Kinadharia .......... 23

2.5.1 Nadharia ya Sosholojia .......... 24

2.5.2 Nadharia ya Simiotiki .......... 26

2.6 Pengo la Maarifa .......... 30

2.7 Hitimisho .......... 31

**SURA YA TATU .......... 32**

**3.0 MBINU ZA UTAFITI .......... 32**

3.1 Utangulizi .......... 32

3.2 Eneo la Utafiti .......... 32

3.3 Usanifu wa Utafiti .......... 32

3.4 Kundi Lengwa .......... 33

3.5 Sampuli na Usampulishaji .......... 34

3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa .......... 35

3.6.1 Data za Msingi .......... 35

3.6.2 Data za Upili .......... 35

3.7 Mbinu za Kukusanya Data .......... 36

3.7.1 Usaili .......... 36

3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka .......... 37

3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data .......... 37

3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo .......... 37

3.9 Usahihi wa Data za Utafiti ........ 38

3.10 Maadili ya Utafiti ........ 38

3.11 Hitimisho ........ 39

**SURA YA NNE ........ 40**

**4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ........ 40**

4.1 Utangulizi ........ 40

4.2 Dhima ya Methali za Kisimbiti ........ 40

4.2.1 Kuacha Tamaa na kuwa na Subira ........ 41

4.2.2 Kuelimisha Jamii ........ 49

4.2.3 Kufanya kazi kwa Juhudi na Maarifa ........ 70

4.2.4 Kuhimiza Umoja na Mshikamano ........ 81

4.2.5 Umuhimu wa Malezi Bora katika Jamii ........ 86

4.3 Mbinu za Kisanaa katika Methali za Kisimbiti ........ 93

4.3.1 Lugha ya Mafumbo katika Methali za Kisimbiti ........ 93

4.3.2 Matumizi ya Takriri ........ 95

4.3.3 Matumizi ya Taswira ........ 97

4.3.4 Muundo katika Methali za Kisimbiti ........ 98

4.4 Hitimisho ........ 99

**SURA YA TANO ........ 100**

**5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO ........ 100**

5.1 Utangulizi ........ 100

5.2 Muhtasari ........ 100

5.2.1 Dhima ya Methali za Jamii ya Wasimbiti na Uhalisia Wake ........ 100

5.2.2 Mbinu za Kisanaa katika Methali za Kisimbiti ............................................ 102

5.3 Hitimisho ................................................................................................. 102

5.4 Mapendekezo ............................................................................................ 103

**MAREJELEO ........................................................................................... 104**

**KIAMBATANISHO .................................................................................. 108**

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Hii ni sura ya kwanza ya utafiti wetu ambapo tumewasilisha vipengele vinavyohusiana na utangulizi. Vipengele hivyo ni historia fupi ya jamii ya Wasimbiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasinifu.

## 1.2 Historia Fupi ya Jamii ya Wasimbiti na Methali Zao

Wasimbiti ni kabila la Tanzania kaskazini magharibi kandokando ya ziwa Viktoria katika wilaya ya Rorya karibu na mpaka wa Tanzania na Kenya. Jamii hii inaongea lugha ya Kisimbiti na wanakadiriwa kuwa 33,000 hivi. Wasimbiti wanazungumza lugha inayokaribiana na Wahasha, Wakine, Wakiroba, Wasurwa na Wasweta. Ndugu zao upande wa Kenya wanaitwa Wasuba.

Jamii nyingi za Maziwa Makuu zina utamaduni wake, kila jamii ina mila na desturi zake. Fasihi Simulizi ndiyo fasihi ya kwanza iliyoanza kutumika pale mwanadamu alipoanza kuishi, hivyo hakuna jamii au kabila ambalo linaendesha maisha yake ya kila siku bila kuzingatia utamaduni wake ambao hutumika katika kudumisha mila na desturi zao, pamoja na kazi zao za kila siku.

Utafiti huu unahusu methali za kabila la Wasimbiti, jamii hiyo inamethali ambazo hutumika kama kipengele cha Fasihi Simulizi. Methali hutumia maneno machache,

kimafumbo au kwa kupigia mifano ili kuelezea maadili na uzoefu wa shughuli mbalimbali katika jamii hiyo, kwa ujumla methali ni hazina kubwa ya mafunzo ya hekima katika tamaduni nyingi za kitanzania. Methali zinatufundisha jinsi ya kuishi katika jamii zetu, namna ya kuwasiliana, kusaidiana, kuhudumiana, kuheshimiana, na kuvumiliana.

Methali ni kama katiba inayomwongoza mtu na kumwelekeza namna ya kuishi na kuenenda na kutenda katika jamii inayomzunguka. Methali inagusa maisha yetu yote, na methali hutukumbusha na kutuhimiza, kulinda na kudumisha tamaduni zetu. Kimapokeo methali zimepokelewa kutoka kizazi hadi kizazi. Wakati wa Babu zetu walipokezana methali hizo kwa njia ya masimulizi tu, utaratibu huo ulitokana na hali halisi iliyokuwepo nyakati hizo, utamaduni wa kusoma na kuandika ulikuwa haujaenea katika sehemu nyingi za Afrika. Lakini siku hizi utamaduni wa kusoma na kuandika umeenea kwa watu wengi, hivyo sasa tunaweza kupokezana mafunzo hayo ya hekima kwa utaratibu wa maandishi mbalimbali na njia nyinginezo za kisasa.

Methali hutumika katika jamii ya Kisimbiti kwa nia mbalimbali hii ni pamoja na kuelimisha, kuonya kuasa na mafunzo mengine. Methali hutumika pia kuboresha mazungumzo ya kawaida na mazungumzo yaliyo rasmi kama vile hotuba katika mihadhara na katika mazungumzo. Methali hutumika pia kufafanua kile kinachoelezwa katika hotuba na kuwa kiini cha mazungumzo yenyewe.Katika mazungumzo ya kawaida methali hutumika kupamba lugha na kufanya mazungumzo hayo yapendeze na kuvutia. Wakati mwingine methali hutumika kama fumbo ili werevu waelewe na wasioelewa wabaki walivyo. Methali hutumiwa zaidi na watu

wazima, hasa wazee na watu wa makamo, pia vijana hutumia methali mara chache sana katika shughuli zao.

Methali za kisimbiti zina manufaa kwa wasomaji na watumiaji kwa sababu zinagusa mazingira na maisha ya jamii hiyo, kwa mfano zipo methali zinazozungumzia maisha ya wakulima mfano wa methali hizo ni kama hii *"ekebhagho ketakutubha molemihë"* (Tar- jama: Jembe halimtupi mkulima), *"singa nekebhagho kyane kera nenakyo, singa nkabhatongirë"* (Tar- jama: Ningekuwa na jembe langu lile dogo ningewazidi/ ningezidisha juhudi ya kulima). Pia zipo methali nyingi mojawapo ni methali zinazozungumzia upendo, umoja na mshikamano katika jamii mfano "*Osore bhonswe tomanyire ono arekhobheka*" (Tar- jama: Jali watu wote si wako tu huwezijua nani atakuzika).

Hii ni mifano michache tu lakini zipo methali nyingi zilizokusanywa na kuandikwa katika utafiti huu ambazo zinagusa sehemu kubwa ya mazingira na maisha ya wasimbiti, hivyo msomaji ataona kuwa methali zilizokusanywa katika utafiti huu ni baadhi ya methali zinazoonekana kuwa ni kongwe na za kale ambazo zimerithishwa kutoka kwa mababu zetu, methali hizi ni kama vile, *"nyakemaamano yarëëyë beno bhetahëëyë"* (Tar- jam: Mwenye uchu alikula chakula kisicho iva). Au *"umwiteki uworo senke, numwene akorotoorä"* (Tar-jama: Anayejitwika mtungi kichwani ni yeye peke yake atakayetua mtungi).

Pia zipo methali ambazo zinaonekana wazi kuwa ni methali mpya kwa kuwa ni methali zilizobuniwa baada ya ujio wa wageni kama Waarabu na Wazungu katika

nchi za Afrika Tanzania ikiwemo (Sengo, 2009). Baadhi ya methali hizo ni *"Ensaho eno ebhosa, tikwi merahë* (Tar-jama: Gunia tupu haliwezikusimama), au *"ikyaraikiyankotorwakere ikitwang'a"* (Tar-jama chanda chema huvikwa pete). Katika utafiti huu methali zimeandikwa katika lugha ya Kisimbiti na kufuatiwa na tar- jama na maana zake katika Kiswahili, hivyo methali hizo zimekaribiana sana na kufanana kwa ukaribu zaidi na methali za Kiswahili.

## 1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Methali ni kijitanzu cha fasihi simulizi ambacho kimekuwepo ulimwenguni tangu pale tu binadamu alipoanza kufanya shughuli za uzalishaji mali na kuwasiliana na wenzake kwa kutumia lugha (Finnegan, 1970). Methali ni aina ya semi ambazo zina busara na hekima ndani yake kiasi cha kuwa ndio chombo cha kutolea elimu katika jamii za Kiafrika kabla na hata baada ya kuja kwa wakoloni kutawala nchi hizi (Njogu na Chimerah, 1999). Baada ya kuja kwa wakoloni na kuanzisha mfumo wa kutoa elimu kwa kutumia shule na madarasa maalumu matumizi ya methali yalipungua kwa kiasi, lakini bado yaliendelea kuwepo kwani elimu hiyo ya kikoloni ilitolewa kwa watu wachache tu.

Kuendelea kutumika kwa methali kama chombo cha mawasiliano na kutolea elimu katika kipindi cha ukoloni kuliambatana na changamoto kadhaa huku kubwa ikiwa ni ile dhana ya wakoloni kuona kila kitu ambacho kinafanywa na Waafrika ni cha kishenzi, kisicho cha kistaarabu na cha watu wajinga (Wamitila, 2008). Hata hivyo, baadhi ya Waafrika hawakukubaliana na mtazamo huo wa wakoloni na badala yake waliendelea kupigania matumizi ya methali kama chombo cha kufundishia na

kutolea elimu katika jamii. Mtafiti wa kwanza kabisa kutoka Ulaya aliyeingia katika bara la Afrika na kufanya utafiti juu ya fasihi simulizi ni Finnegan (1970). Mtafiti huyu anakiri kwamba jamii zote za Afrika zina utajiri wa methali nyingi ambazo kwazo ndimo mna maadili, hekima na busara na miongozo mbalimbali ya maisha.

Methali ni kijitanzu hai cha fasihi simulizi kwani huzaliwa kila siku kulingana na matukio mbalimbali yanayotokea katika maisha ya kila siku ya jamii (Madumulla, 2005). Mwanadamu ni mtu ambaye amekuwa akijishughulisha katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na ni katika shughuli hizo amekuwa akiibua methali zenye mafunzo na elimu kubwa kwa jamii (Alzarock, 2016). Jamii ya Wasimbiti wanaoishi katika wilaya ya Rorya mkoani Mara ni moja kati ya jamii zaidi ya 120 za makabila ya Tanzania ambayo ina utajiri wa methali nyingi. Methali katika jamii hii zimekuwa na dhima tofautitofauti kama vile kufundisha, kuonya, kuadilisha, kuburudisha, kulea, kuhimiza uwajibikaji, na kuhamasisha umoja na mshikamano katika jamii.

Umuhimu huu wa methali za jamii ya Wasimbiti ni sawa kabisa na ule wa methali katika makabila mengine ya duniani, Afrika na Tanzania. Watafiti kadhaa kama vile Mohammad (1998) aliyechunguza nafasi ya mwanamke katika methali za jamii ya Iraq, Mohammad (1999) aliyechunguza methali katika jimbo la Darfur huko Sudani, Hussein (2000) aliyechunguza methali huko Jordan, Mphande (2001) aliyechunguza methali za jamii ya Tonga huko Malawi na Ahmed (2005) aliyechunguza methali za jamii ya Sudan na kulinganisha na methali za Uingereza wanakiri kwamba dhima ya methali ni ile ile duniani kote. Watafiti hawa wanabainisha kuwa methali za jamii

hizo walizozitafiti zinafanana katika mambo mengi ikiwa ni pamoja na namna zinavyomtazama mwanamke.

Kimsingi, Methali duniani kote zinamtazama mwanamke kama kiumbe duni ambaye hastahili kupewa fursa za uongozi na kuishia kuwa ni kiumbe wa ndani ambaye kazi yake kubwa ni kumhudumia mwanaume. Methali za jamii za Kitanzania pia zina dhima zinazofanana katika kila nyanja ya maisha. Hili linathibitishwa na utafiti uliofanywa na Mwenerwa (2003) aliyechunguza methali za Wahaya, Senzighe (2004) aliyechunguza methali za Wapare, Bwanamaya (2004) aliyechunguza methali za Wakerewe na Madumulla (2005) aliyechunguza methali za Wahehe. Methali zote hizi zina dhima zilezile za kuelimisha, kuburudisha, kuhamasisha uwajibikaji, kuhimiza umoja na mshikamano na kupendana miongoni mwa wanajamii. Wakati baadhi ya methali za jamii mbalimbali duniani zikiwa zimetafitiwa kwa kiasi fulani, methali za jamii ya Wasimbiti bado hazikutafitiwa kwa namna yoyote ile hata kukusanywa au kutajwa tu kuwa katika jamii ya Wasimbiti kuna methali. Utafiti huu ulifanywa kutokana na ukweli huo kwa lengo la kuchunguza dhima za methali hizo.

## 1.4 Tatizo la Utafiti

Jamii ya Wasimbiti imekuwa na methali tangu pale Wasimbiti walipoanza kuwasiliana kwa kutumia lugha yao ya Kisimbiti. Wamekuwa wakitumia methali kama chombo cha kuwasiliana, kutolea elimu na kushajiishana katika kufanya kazi. Dhima hii ya methali imekuwa ni ya dunia nzima na si kwa jamii ya Wasimbiti peke yake. Mawazo haya yanathibitishwa na Finnegan (1970) aliyechunguza fasihi simulizi ya Kiafrika. Watafiti kadhaa wamevutiwa katika kufanya utafiti juu ya

methali za makabila ya Tanzania kwa malengo na mikabala tofautitofauti. Miongoni mwao ni Mwenerwa (2003) ambaye alichunguza namna methali za Kihaya zilivyoathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, Senzighe (2004) ambaye alichunguza nafasi ya mwanamke katika methali za Wapare na Madumulla (2005) aliyechunguza methali za kabila la Wahehe. Kati ya watafiti wote hawa hakuna aliyetafiti methali za jamii ya Wasimbiti wa wilayani Rorya mkoani Mara ili kubaini dhima ya methali katika jamii ya Wasimbiti. Utafiti huu ulifanywa ili kuziba pengo hili la maarifa.

## 1.5 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu moja na malengo mahususi matatu kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza dhima za methali za jamii ya Wasimbiti.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:

a) Kubainisha dhima zinzopatikana katika methali za jamii ya Wasimbiti wa wilaya ya Rorya huko mkoani Mara.

b) Kufafanua uhalisia wa dhima zinazopatikana katika methali za jamii ya Wasimbiti kwa jamii ya leo.

c) Kuelezea mbinu za kisanaa zinazotumika kujenga dhima katika methali za jamii ya Wasimbiti wa wilayani Rorya mkoani Mara.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti huu ni:

a) Ni dhima zipi zinazopatikana katika methali za jamii ya Wasimbiti wa wilaya ya Rorya mkoani Mara?

b) Dhima zilizopo katika methali za jamii ya Wasimbiti zina uhalisia gani kwa jamii ya leo?

c) Dhima katika methali za jamii ya Wasimbiti wa wilaya ya Rorya mkoani Mara zinajengwa kwa kutumia mbinu zipi za kisanaa?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu sana kwani utakuwa umefanya jambo ambalo haliwezi kusahaulika kihistoria. Methali za makabila mengi ya Kiafrika zimesheheni utajiri mkubwa wa amali, maadili, hekima na busara lakini hazihifadhiwi vizuri katika maandishi. Kupitia utafiti huu methali za Kisimbiti zimekusanywa, kuchambuliwa na kuandikwa katika tasinifu kwa ajili ya kujisomea vizazi na vizazi katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kwa upande wa jamii ya Wasimbiti, watauona utafiti huu kuwa na maana kubwa sana kwao kutokana na kule kutafiti methali zao. Baadhi ya wanajamii wameshapata ile dhana ya kudharau mila na desturi za makabila zikiwemo methali, kupitia utafiti huu wataona kumbe methali bado zinathamani kubwa hata zinatafitiwa na wataalamu kutoka chuo kikuu.

Utafiti huu pia utakuwa ni moja kati ya marejeo muhimu ambayo yatatumiwa na watafiti wa sasa na wa baadae katika kuimarisha tafiti zao. Kutokana na utafiti huu

wanaweza kupata mawazo ya kufanya utafiti zaidi katika methali za makabila mbalimbali ya Tanzania na hata nje ya Tanzania. Walimu na wahadhiri wa vyuo na vyuo vikuu watautumia utafiti huu katika kuandaa maalumati ya masomo yao ili kufundisha kwa ufanisi somo la fasihi simulizi.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unahusu methali za jamii ya Wasimbiti wanaopatikana katika kata ya Komuge iliyoko katika wilaya ya Rorya kupitia vijiji vya Kyabhaibi, Kinesi, Iryenyi na Songambele. Wilaya ya Rorya ina kata na vijiji vingi tu lakini sisi tumeamua kuchagua kata na vijiji tajwa tu kwa sababu ndivyo vilivyoweza kutupatia data za utafiti tulizozihitaji.

## 1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii itakuwa na jumla ya sura tano ambapo sura ya kwanza ilikuwa inatoa utangulizi wa tasinifu nzima. Utangulizi huo umetolewa kupitia vipengele vya historia fupi ya Wasimbiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasinifu. Baada ya hapo ilifuata sura ya pili ambayo iliwasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu imewasilisha mbinu za kukusanya na kuchambua data na sura ya nne ikiwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti. Sura ya tano imetoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imefanya kazi ya kupitia kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti pamoja na mkabala wa kinadharia. Lengo la sura hii lilikuwa ni kujaribu kutazama watafiti watangulizi wanasema nini kuhusiana na mada ya utafiti huu. Kwa jumla tumeweza kubaini kwamba hakuna mtafiti hata mmoja ambaye amewahi kufanya utafiti wa kuchunguza methali za jamii ya Wasimbiti wanaoishi katika wilaya ya Rorya mkoani Mara. Hili limeweza kufahamika baada ya kupitia kazi tangulizi zinazohusiana na utafiti wa methali duniani, fani katika methali na utafiti tangulizi katika methali za Tanzania.

## 2.2 Utafiti wa Methali Duniani

Methali ni aina ya misemo ambayo huwa na pande mbili, upande wa kwanza huwa ni kama swali na upande wa pili huwa ni majibu ya swali lililoulizwa. Methali hupatikana katika jamii zote duniani kutokana na umuhimu wake katika jamii. Methali ndizo ambazo hutumika katika kurithisha mila, desturi, busara na hekima katika jamii iliyopita, iliyopo na ijayo (Mulokozi, 1996). Kutokana na kuwepo kwake duniani kote, utafiti umekuwa ukifanyika kuchunguza masuala mbalimbali yanayohusiana na methali hasa katika vipengele vya fani na maudhui kwa mtazamo wa fasihi. Pia wapo wataalamu wa taaluma za Sosholojia na Saikolojia ambao nao pia wamekuwa wakichunguza methali kwa namna moja au nyingine kulingana na mawanda ya taaluma zao. Kwa upande wa fasihi, wapo wataalamu kadhaa ambao

wamefanya utafiti juu ya methali sehemu mbalimbali duniani ambao tumepitia kazi zao hapa chini kama ifuatavyo:

Mtaalamu wa fasihi duniani anayejulikana kwa jina la Finnegan (1970) alifanya utafiti kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika na kufanikiwa kuandika kitabu kilichoitwa *Oral Literature in Africa*. Kitabu hiki kimezungukia fasihi simulizi kwa ujumla wake na utanzu wa semi nao ukielezwa kinagaubaga. Katika maandishi yake anaeleza methali ni moja kati ya kijitanzu cha fasihi simulizi ambacho kinajitokeza katika mataifa yote ya Afrika. Itakumbukwa kuwa katika Afrika hakukuwa na mfumo rasmi wa kutolea elimu kama ule ulioletwa na wakoloni wa kujenga shule na wanafunzi kuingia darasani na kisha kufundishwa na mwalimu aliyehitimu masomo ya ualimu. Hivyo, methali zilitumika kama chombo cha kutolea elimu kwa wanajamii. Hii ni kwa sababu methali ni maneno yenye hekima na busara ambayo hutumika kumwelekeza mtu katika njia iliyonyooka. Hali kama hii imekuwepo pia katika jamii ya Wasimbiti wanaopatikana katika wilaya ya Rorya mkoni Mara. Katika jamii hii, methali zimekuwepo tangu enzi na enzi na zimekuwa zikifanya kazi kama hii inayotajwa na Finnegan (1970). Hata hivyo, mpaka kufikia hivi sasa hakuna utafiti ambao umefanyika katika kuchunguza dhima za methali hizo. Jambo hili lilitusukuma kufanya utafiti ili tuweze kukusanya methali za Kisimbiti na kisha kuzichambua ili kutimiza malengo ya utafiti wetu.

Knappert (1977) alifanya utafiti uliolenga kuchunguza dhamira zinazojitokeza katika methali za jamii za Waafria na kufanikiwa kutoa kitabu. Katika kitabu chake hicho ameeleza mambo mengi lakini kubwa likiwa ni kwamba suala la imani ya dini hasa

dini za kimila linajitokeza sana katika methali za jamii ya Waswahili. Anasema kwamba, ukitaka kufahamu vizuri juu ya imani kwa Waafrika tazama methali zao. Katika methali zao utaona namna waafrika wanavyomuogopa Mungu ambaye wao kwa mujibu wa mila zao wanamuamini kuwa ni Mungu. Kutokana na imani ya dini, jamii nyingi za Waafrika zimekuwa zikihimizana kufanya mambo mema na kuacha mambo mabaya. Mawazo haya yanaungwa mkono na Mbiti (1996) ambaye anazungumza juu ya taaluma ya Filosofia katika nchi za Afrika ambapo anasema kwamba, imani juu ya dini ni moja kati ya mambo muhimu yanayopewa nafasi kubwa na Waafrika katika maisha yao ya kila siku. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwani hata sisi katika uzoefu wetu tunashuhudia kwamba ni kweli wanajamii wamemakinikia sana imani za dini zao. Katika kuthibitisha hili ni pale ambapo mtu fulani atakapojaribu kukashifu au kudhalilisha dini ya mtu mwingine. Jamii ya Wasimbiti nayo haiko nyuma katika kuamini masuala mbalimbali ya kidini na imani yao inathibitika vizuri katika methali zao. Katika utafiti huu tumechunguza suala la imani katika dini pamoja na mafundisho ya kidini yanavyojitokeza katika methali za jamii ya Wasimbiti.

Oniango (1978) alikusanya methali za jamii ya Waluya wa nchini Kenya na kuzifanyia uchambuzi. Katika kazi yake hii anasema kwamba, jamii ya Waluya ina utajiri mkubwa wa methali zenye kuzungumzia masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Moja kati ya mambo muhimu yanayoelezwa katika methali hizo umoja na mshikamano kuwa ni jambo muhimu katika kufanikisha maendeleo ya jamii. Waluya wanaamini kwamba hakuna jambo lolote ambalo linaweza kufanikiwa vizuri kama wanajamii watakuwa hawana umoja na mshikamano baina yao. Imani

hii inajitokeza katika methali za jamii mbalimbali za Afrika na hata Waswahili wanayo methali isemayo, “umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.” Hii inaonyesha kuwa umoja ni kitu muhimu sana katika kufanikisha masuala ya maendeleo katika jamii. Maelezo haya ni sahihi hasa ikikumbukwa kwamba maisha ya zamani hayakuwa na tekinolojia ambayo tunayo hivi sasa ambapo mambo mengi yamerahisishwa kwa kufanywa na mashine. Maisha ya zamani yalitegemea sana umoja na msikamano katika kufanya mambo mbalimbali ya uzalishaji mali kama kilimo ambacho ndio shughuli kubwa ya uzalishaji mali katika jamii nyingi za Kiafrika tangu kale mpaka leo. Hata hivyo, suala la umoja na mshikamano bado lina umuhimu mkubwa kwa maisha ya leo kwani mambo mengi yanahitaji nguvu ya pamoja ili kufanikiwa. Katika utafiti wetu tumechunguza ni kwa vipi katika jamii ya Wasimbiti wanadumisha dhana ya umoja na msikamano katika methali zao.

Methali ni kijitanzu cha fasihi simulizi ambacho kinabeba masuala mbalimbali yanayohusu jamii licha ya kuwa methali huandikwa kwa sentensi moja inayoenea katika msitari mmoja tu au hata nusu msitari (Maitaria, 2012). Mawazo haya ya Maitaria yalishawahi kutolewa pia na Mohammad (1999) ambaye alitafiti nafasi ya mwanamke katika methali za jamii ya Darfur katika nchi ya Sudan. Anabainisha kwamba katika jamii yake zipo methali ambazo zinamzungumzia mwanamke katika hali chanya na duni lakini zile zenye mtazamo wa uduni ni nyingi zaidi. Mawazo haya ni sahihi kwani katika jamii nyingi duniani mwanamke amekuwa akisawiriwa katika hali ya uduni katika maeneo mengi ikilinganishwa na mwanaume ambaye anasawiriwa katika hali chanya. Hali hii ya kumsawiri mwanamke kama kiumbe duni inaonekana kuwa ni suala la kiulimwengu na huenda likawa limechangiwa na

mambo mengi ikiwemo dini na imani katika mila na desturi. Mawazo haya tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu kwa lengo la kutazama dhima zinazomgusa mwanamke na mwanaume katika methali za jamii ya wasimbiti na kwa nini hasa mwanamke anasawiriwa katika hali hiyo.

Mtaalamu mwingine ambaye ametafiti juu ya methali katika Afrika ni Mphande (2001) ambaye alichunguza methali za jamii ya Tonga inayopatikana katika nchi ya Malawi. Katika utafiti wake aligundua kuwa methali ni kijitanzu cha fasihi ambacho kinapewa nafasi kubwa sana na wanajamii ya Tonga kutokana na umuhimu wake katika kutoa elimu kwa jamii. Hata hivyo, alibaini kwamba, methali hutumiwa zaidi na wazee kuliko vijana na hivyo kuhatarisha kudumu kwa methali za zamani ambazo bado zinatoa mafunzo muhimu kwa mustakabali wa jamii. Mawazo haya ni ya kweli kwani ni ukweli usiopingika kwamba methali ni chombo muhimu katika kutoa elimu, maonyo na kuimarisha hekima na busara katika jamii hivyo zinahitaji kudumishwa na kuhifadhiwa vizuri.

Ukweli huu unaonekana katika jamii nyingi duniani ambapo tunaona methali za makabila mbalimbali zikipotea kutokana na kutohifadhiwa katika maadishi na watumiaji wakiwa ni wazee ambao wanaondoka duniani mmojammoja na wanakaribia kwisha. Maelezo haya yalitufungua uelewa wetu na kuweza kubaini kwamba kumbe nasi pia tunao wajibu wa kutafiti methali za jamii ya Wasimbiti na kuzihifadhi katika maandishi ili zisipotee moja kwa moja. Hivyo basi tumefanya utafiti huu na kufanikiwa kukusanya methali za jamii ya Wasimbiti na kuhifadhi katika maandishi ambapo vizazi na vizazi vitazisoma na kuzitumia.

Alzarock (2016) alimdondoa Ahmed (2005) ambaye alifanya utafiti uliolinganisha methali za jamii ya watu wa Sudan na Uingereza. Katika utafiti huo alibaini kwamba jamii zote mbili zina matumizi ya methali licha ya kuwa jamii moja ni ya nchi ya kimasikini na jamii nyingine ni ya nchi iliyoendelea. Alibaini kwamba methali za jamii zote mbili zinaundwa kwa kuwa na pande mbili ambapo upande mmoja huwa ni kama swali na upande wa pili huwa ni jibu la swali lililoulizwa. Pia alibaini kwamba, methali za jamii zote mbili zinamsawiri mwanamke katika hali chanya na hali hasi, lakini hali hasi ndiyo inayotawala zaidi. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwa sababu ni katika methali nyingi duniani mwanamke amekuwa akisawiriwa kama kiumbe duni ambaye ni tegemezi kwa mwanaume, mfitinishaji, malaya, asiye na uvumilivu, asiye na busara na asiyekuwa na uwezo wa kupatiwa uongozi. Maelezo haya tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu juu ya methali za jamii ya Wasimbiti.

## 2.3 Mbinu za Kisanaa katika Methali

Kama tulivyoeleza hapo awali kuwa methali ni kijitanzu cha fasihi simulizi ambacho kinapatikana katika utanzu maarufu wa semi. Vijitanzu vingine katika utanzu wa semi ni vitendawili, misemo, nahau na misimo (Mulokozi, 1996). Hivyo, kama kijitanzu cha fasihi kimesheheni mbinu za kisanaa ambazo ndizo zitumikazo kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa.

Methali ni chombo cha mawasiliano ambacho hutumia katika kupashana habari miongoni mwa wanajamii. Maitaria (1991) katika utafiti wake anasema kwamba methali ni chombo chenye dhima kubwa katika kuipasha jamii habari mbalimbali

zinazohusiana na maisha yao. Hii ni kutokana na ukweli kuwa methali ni zao la jamii na hivyo kile kinachosemwa katika methali ni kitu chenye uhakika na hakina mashaka. Hivyo, methali hutumia lugha ambayo hueleweka kwa jamii husika bila matatizo kwa sababu jambo linalosemwa katika methali wanalifahamu. Hii haina maana kwamba methali zote hutumia lugha ya wazi yenye kueleweka moja kwa moja bila hata kutafakari kidogo. Zipo methali ambazo hutumia lugha ya mafumbo, ishara, picha na taswira ambazo wakati mwingine zitaihitaji hadhira kutafakari kidogo kabla ya kuelewa ni nini kinachosemwa katika methali husika. Kwa mfano, katika Kiswahili kuna methali isemayo "ganda la muwa la jana, chungu kaona kivuno." Methali hii imetumia lugha ya picha kwani anayesemwa hapa si chungu bali ni binadamu, kwamba inaweza ikafika mahali mtu akawa na utajiri unaomuwezesha kupata kila kitu anachokihitaji katika maisha hata akafikia kufanya isirafu. Baada ya muda utajiri alionao unaweza ukatoweka na akakumbuka vitu alivyokuwa anavifanyia isirafu asivipate na akaishia kuishi maisha ambayo ni dhalili kabisa. Matumizi ya lugha ya namna hii tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika utafiti wetu uliochunguza dhamira na dhima katika methali za jamii ya Wasimbiti.

Mulokozi (1996) anatueleza kuwa methali zimeundwa na vipengele vya fani na maudhui kama ilivyo katika kazi nyingine za fasihi kama ushairi, riwaya, tamthiliya, hadithi na sanaa za maonesho. Anaendelea kueleza kwamba, moja kati ya vipengele vya kisanaa vinavyojitokeza katika methali matumizi ya mbinu za kishairi za vina na mizani. Methali nyingi zimeundwa kwa kutumia mtindo huo wa vina na mizani kama njia ya kutoa msisitizo katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira. Kwa mfano kuna methali ya Kiswahili inayosema, "haba na haba, hujaza kibaba," tunaona kipengele

cha kina cha kati na cha mwisho vinafanana. Kina hicho ni “ba” ambacho si tu kwamba kinatia ladha katika kutamkwa bali pia kinatoa msisitizo fulani kwa hadhira katika kutilia maanani jambo linaloelezwa mbele yao.

Sambamba na matumizi ya vina katika methali hiyo pia kuna matumizi ya takriri, ambapo neno “haba” limerudiwa mara mbili. Marudirudio ya neno hili yameifanya methali kuonekana kuwa jambo inalolisemea ni muhimu sana na kila mwanajamii anapaswa kulizingatia. Hii tunaita ni takriri neno, lakini pia kuna takriri silabi katika methali hiyo ambapo silabi “ba” imejitokeza mara tatu katika methali hiyo. Maelezo haya yanaonesha kwamba katika methali kuna utajiri mkubwa wa matumizi ya mbinu za kisanaa kwani katika methali moja kunajitokeza mbinu zaidi ya moja. Katika utafiti wetu, tumeyatumia maarifa haya kwa lengo la kubaini namna matumizi ya mbinu za kisanaa yanavyotumika katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa.

Njogu na Chimerah (1999) ni kati ya wataalamu wa fasihi ya Kiswahili ambao wameandika kuhusu kijitanzu cha methali. Wanasema kwamba, methali ni misemo ambayo imetungwa kitaalamu kana kwamba waliotunga methali hizo ni wasomi wa hali ya juu lakini kumbe ni watu wa kawaida tu katika jamii. Ukitaka kuthibitisha kuwa methali zimetungwa kitaalamu ni pale ambapo utajaribu kutunga methali yako ya aina yoyote ile lakini usiweze. Maelezo ya wataalamu hawa yanathibitisha kwamba methali si misemo ya kawaida bali ni misemo ambayo ni ya kitaalamu na inafanya kazi ya kuelimisha na kuburudisha jamii. Kimsingi, utunzi wa methali katika ulimwengu wa fasihi simulizi huwa hauna muda maalumu kwamba sasa mtu

fulani amekaa chini tayari kwa ajili ya kutunga methali. Methali huibuliwa kulingana na mazingira maalumu. Kwa kulielewa suala hili imekuwa kazi rahisi kwetu kukusanya methali za jamii ya Wasimbiti kutoka kwa watu mbalimbali wanaojua methali. Kama ingekuwa methali hutungwa na watu maalumu ingekuwa ni vigumu kupata methali hizo kwani wamiliki wangehitaji fedha ndipo watupatie methali.

Methali ni kijitanzu ambacho kinaweza kutumiwa kama mbinu ya kisanaa katika kazi nyingine za fasihi ulimwenguni (Senkoro, 2006). Mtaalamu huyu anaeleza kuwa methali hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi andishi kama tamthiliya kuwa ni majina ya tamthiliya hizo. Mfano, mzuri ni tamthiliya ya *Lina Ubani* iliyotungwa na Penina Mlama. Jina hili la tamthiliya linatokana na methali ya Kiswahili iitwayo, "la kuvunda halina ubani," sasa hapa mtunzi yeye anasema "Lina Ubani." Hiki ni kinyume cha methali hiyo ambacho kimetumiwa kisanaa. Msomaji wa kazi hiyo anapokutana na maneno kama haya kwa mara ya kwanza atajiuliza kuwa kwa nini jina la tamthiliya hii linasomeka hivyo? Katika kutafakari kwake anaweza kuipata vizuri baadhi ya dhamira ambazo zinajitokeza katika tamthiliya hii. Mawazo haya ya Senkoro ni muhimu sana katika kupeleka mbele utafiti wetu kwani yametupatia ufahamu kwamba, methali huandikwa kwa maneno machache lakini ndani mwake mna utajiri mkubwa wa dhamira ambazo ni muhimu kwa maisha ya jamii. Ufahamu huu umetufanya kuwa makini katika kuichunguza kila methali kwa makini ili tuweze kuyaona maarifa mengi yanayopatikana ndani ya methali husika.

Kunnemah (2007) amekuwa na mawazo kama yale ya Senkoro (2006) lakini yeye anazungumza juu ya methali kutumika kama jina la shairi. Anaeleza kuwa si jambo

la ajabu kukutana na jina shairi ndani ya kitabu cha mashairi lisomekalo, “kikulacho,” na majibu yake ambayo ni “kinguoni mwako yanaonekana katika beti za shairi husika. Hii inaonesha kuwa methali ni mbinu ya kisanaa ambayo inaweza kutumika katika kuandaa kazi nyingine za fasihi na kutengeneza kitu kinachoitwa Muingiliano wa tanzu. Kama tulivyojifunza kuhusiana na mawazo ya Senkoro (2006) ndivyo hivyo hivyo tulivyojifunza katika kazi ya Kunnemah na mafunzo hayo tumeyafanyia kazi katika utafiti wetu.

Wamitila (2008) ameandika kuhusu kijitanzu cha methali na kutoa hitimisho kwamba licha ya kuwa methali ni chombo muhimu cha kupashana habari na kuelimisha ulimwengu lakini bado hazijafanyiwa utafiti wa kutosha. Wataalamu wengi wamekuwa wakimanikia kufanya utafiti katika kazi za fasihi andishi kama riwaya, ushairi na tamthiliya na kusahau kuwa kuna methali ambazo pia zinaweza kutafitiwa.

Mawazo haya tunakubaliana nayo kwa msingi kwamba, baadhi ya wataalamu huona kuwa methali ni kitu kidogo ambacho huandikwa kwa msitari mmoja na wakati mwingine nusu msitari na hivyo kutokuwa na mambo mengi ya kutafiti katika methali. Kwa hakika huu ni mtazamo ambao ni finyu kwani methali zimejaa mambo mengi ambayo yanaweza kuchunguzwa kitaaluma na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya taaluma ya fasihi. Jambo hili lilitusukuma kufanya utafiti katika methali za jamii ya Wasimbiti ili kuweza kuibua maarifa kuntu yanayopatikana katika methali hizo kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae.

## 2.4 Kazi Tangulizi za Methali za Kitanzania

Methali katika jamii ya Watanzania bado ni kipengele ambacho hakijafanyiwa utafiti wa kutosha ikilinganishwa na kazi nyingine za fasihi. Sababu hasa za msingi hazijulikani ila tu ni kama vile alivyosema Wamitila (2008) kuwa wataalamu wengi hudhani kuwa methali hazina mambo mengi ambayo yanaweza kutafitiwa na kuchunguzwa. Hata hivyo, wapo wataalamu kadhaa kama vile Chacha (1999) ambaye alikusanya methali za jamii ya Wakurya wanaishi katika mkoa wa Mara na kuzifanyia uchambuzi. Katika uchambuzi wake anaeleza kuwa methali za jamii ya Wakurya zina utajiri mkubwa wa dhamira zinazohusu, malezi, kuwajibika katika kufanya kazi, kuimarisha umoja na mshikamano, kupendana na kusaidiana katika shida na raha.

Utafiti huu wa Chacha umekwenda mbali na kuonesha kuwa mafundisho ya hekima na busara kwa jamii ya Wakurya yanapatikana katika methali zao na watu wa zamani ambao wengi wao sasa ni wazee walipata elimu yao kupitia methali na si katika shule kama ilivyo hivi sasa. Mawazo haya tumechukuwa na kuyafanyia kazi kwani jamii ya Wasimbiti iko karibu sana na jamii ya Wakurya na hivyo yapo mambo ambayo yanajitokeza katika methali za jamii zote.

Maendeleo ya Sayansi na tekinolojia yana mchango mkubwa katika kudidimiza methali za makabila ya Tanzania kuliko mchango wa kuendeleza na kudumisha methali hizo (Mwenerwa, 2003). Mwanataaluma huyu anaeleza kuwa teknolojia imechangia sana kudunisha methali za jamii ya Wahaya ambapo methali huonekana kuwa ni kitu ambacho kimepitwa na wakati. Hii inatokana na watu wengi kukimbilia

na kudhamini kazi za fasihi ambazo zinaoneshwa katika televisheni na mitandao ya kijamii na kuzipa methali kisogo kana kwamba hazipo kabisa katika jamii hiyo. Baadhi ya wanajamii huziona methali kama ni vitu vya utamaduni wa kizamani sana vilivyoitwa na wageni kuwa ni vya kishenzi. Mawazo haya ni ya kweli tupu kwani hivi sasa si katika yamii ya Wahaya pekee bali katika jamii nyingi za Kiafrika methali zimesahaulika na kushushwa thamani yake. Hili ndilo jambo ambalo limetusukuma kufanya utafiti huu ili hatimaye tuweze kukusanya na kuchambua methali za jamii ya Wasimbiti kwa lengo la kuonesha umuhimu wa methali hizo na kuzihifadhi katika maandishi kwa ajili ya matumizi ya vizazi vijavyo.

Mtaalamu Senzighe (2004) alifanya utafiti uliolenga kuchunguza methali za jamii ya Wapare katika kipengele cha jinsia na kugundua kuwa methali hizo zinaikandamiza jinsia ya kike. Anaeleza kuwa katika methali za Kipare mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye hawezi kuwa na uelewa wa kutoa mawazo mazuri ya kuipeleka mbele jamii yake na badala yake huwa ni msikilizaji tu way ale yanayosemwa na wanaume. Hii ina maana kuwa, mwanamke hapewi nafasi ya kushiriki katika maamuzi muhimu yanayofanyika katika jamii yake na hivyo yale mambo ambayo yanamlenga moja kwa moja kama mwanamke yanakosa kupatiwa masuluhisho muafaka. Mawazo ya Senzighe ni ya kweli na yanajitokeza katika methali za jamii nyingi duniani kutokana na kutawala kwa mfumo dume uliopo katika jamii.

Mfumo dume humuona mwanaume kuwa ndiye mwenye akili na maarifa ya kuweza kutoa maamuzi sahihi juu ya masuala yahusuyo familia na hata taifa. Mawazo haya

tumeyachukuwa na kuyafanyia kazi katika tasinifu yetu, kwani yameufungua uelewa wetu juu ya nafasi ya mwanamke katika methali za makabila ya Tanzania.

Bwanamaya (2004) alifanya utafiti uliochunguza uhusiano uliopo baina ya mabadiliko katika jamii na methali katika jamii ya Wakerewe. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa mabadiliko yanayotokea katika jamii hususani kutokana na kuingiliana kwa jamii moja na nyingine kuna changia sana kupotea kwa methali katika jamii ya Wakerewe. Wakerewe walipokuwa wakiishi peke yao bila maingiliano na jamii nyingine za Tanzania walikuwa wakitumia methali zao kwa kiasi kikubwa kama chombo cha kufundisha mema na kukataza mambo mabaya katika jamii yao. Hivi sasa jamii ya Wakerewe inaishi pamoja na mchanganyiko wa jamii nyingi na hivyo matumizi ya lugha ya Kikerewe na methali zake ni ndogo sana. Mawazo haya yanajitokeza kuthibitisha yale yanayotokea katika jamii nyingi za Kitanzania kwani bado mwingiliano wa jamii umesababisha mambo mengi ya kimila ya jamii hizo kupotea. Hivyo, tumeamua kufanya utafiti huu kama sehemu ya mchango wetu katika kuhifadhi na kutunza utamaduni wa jamii ya Wasimbiti kupitia methali zake.

Madumulla (2005) amefanya utafiti katika kabila la Wahehe, ametafiti methali za kihehe na kubaini kuwa kuna methali za kihehe zinazohusisha ndege, vifo, uwindaji, Mungu, miti, maisha, wadudu, wanawake, wanaume, wachawi na hata magonjwa. Katika maelezo yake anabainisha kuwa, pamoja kwamba kuna methali kama alivyozigawanya katika makundi haya lakini methali zote zipo kwa ajili ya kutoa elimu ya kumfundisha binadamu namna bora ya kuweza kuishi na wanadamu

wenzake. Mawazo haya tunakubaliana nayo kwamba ni kweli jamii nyingi ikiwemo ile ya Wasimbiti wanazo methali ambazo huzungumza juu ya vitu tofautitofauti lakini mlengwa hasa ni binadamu. Tumeyachukuwa mawazo haya na kuyafanyia kazi kwa kina ili kuweza kuona namna methali za Wasimbiti nazo zinavyotumia methali za aina kama hiyo kutoa elimu kwa hadhira iliyolengwa.

Kwa jumla kazi tangulizi hizi tulizozipitia zinaonesha kuwa methali ni kijitanzu muhimu katika kutoa elimu na mafunzo kwa jamii za makabila yote ya Tanzania. Wakati ambapo hakukuwa na shule kwa utaratibu uliopo hivi sasa, methali zilitumika katika kutoa elimu na kuifunza jamii mambo mbalimbali kuhusu maisha.

Pia katika kazi tangulizi tulizozipitia hakuna mtafiti hata mmoja ambaye ametafiti methali za Wasimbiti kwa namna yeyote ile kama vile kuzikusanya tu au kuzifanyia uchambuzi. Hii imetupa nguvu ya kuufanya utafiti huu ili nasi tuweze kutoa mchango wetu katika kutunza methali za jamii ya Wasimbiti huku tukitoa elimu si tu kwa Wasimbiti bali pia kwa jamii pana zaidi ya Tanzania na duniani kote.

## 2.5 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni mpangilio maalumu unaeleza namna jambo lilivyo, linavyotakiwa kuwa na lilivyokuwa. Nadharia ni muongozo unaelekeza namna ya kufanya mambo kwa ufanisi na tija ili kuimarisha maisha ya mwanadamu. Katika maisha hakuna jambo lolote lile linalofanywa bila ya kuongozwa na nadharia fulani. Mambo yote yawe mema au mabaya hufanywa kwa kuongozwa na nadharia aidha kwa mfanyaji kujua au kutojua. Hivyo katika utafiti wetu ni lazima tuongozwe na nadharia ili tuweze

kutoa kitu ambacho kitakuwa na manufaa kwa jamii. Katika utafiti huu tutatumia nadharia mbili ambazo ni nadharia ya Sosholojia na Simiotiki.

### 2.5.1 Nadharia ya Sosholojia

Sosholojia ni taaluma inayohusu uchunguzi wa jamii katika masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni (Scott, 1999). Sosholojia ni taaluma pana ambayo inaingia katika taaluma nyingine kama vile sayansi ya siasa, saikolojia, uchumi, maendeleo ya jamii, utawala, sheria na kadhalika. Nadharia hii inahusu mahusiano yaliyopo katika jamii na mfumo mzima wa matabaka ya watu kama yanavyopatikana katika jamii husika (Webster, 2006). Masuala ya watu walio nacho ambao hujulikana kama matajiri na wasionacho wanaojulikana kama masikini huelezwa vizuri katika nadharia hii. Matatizo ya wizi, ulevi, utumiaji wa madawa ya kulevya, magonjwa hatari kama UKIMWI na majanga kama ukame na mafuriko pia huelezwa katika nadharia hii.

Vile vile, masuala yanayohusiana na mahusiano ya ndoa na mapenzi kabla ya ndoa na athari zake pia yanaelezwa katika ndharia hii. Masuala ya mila, desturi na dini pia yanaelezwa katika nadharia ya Sosholojia kuwa yana umuhimu sana katika kukuza na kuendeleza jamii yoyote ile duniani na hayapaswi kudharauliwa hata kidogo (Cross, 2011). Nadharia hii pia inazungumzia kuhusu malezi ya watoto kuwa ni jukumu la walezi kuhakikisha kuwa watoto wao wanapata malezi bora ili waje wawe viongozi bora wa baadae.

Muasisi wa nadharia hii ni Adam Smith ambaye aliibua nadharia hii katika kipindi cha mapinduzi ya viwanda huko Ulaya. Katika kipindi cha mapinduzi ya viwanda

huko Ulaya kuliibuka matatizo mengi kwa wakati mmoja na hivyo kuhitaji kuwepo kwa nadharia mbalimbali za kuelezea matatizo hayo (Skeggs, 1997). Matatizo hayo ni kama vile, watumishi wa viwandani kufanyishwa kazi nyingi kwa muda mwingi na malipo kidogo, matatizo ya njaa, kila kitu kuwa bidhaa na hivyo kuhitaji fedha ili kupata mahitaji, unyonyaji wa kikoloni na mengi mengineyo. Nadharia ya Sosholojia iliibuliwa ili iweze kusaidia kuyafahamu vizuri matatizo haya na kuyapatia ufumbuzi wa kudumu.

Hivyo, nadharia hii iliwezesha kupatikana kwa masuluhisho kadhaa ya kutatua matatizo yaliyosababishwa na mapinduzi ya viwanada huko Ulaya (Swingewood, 2000). Kwa mfano, kuhusu wafanyakazi kufanyishwa kazi nyingi kwa malipo kidogo iliamriwa kwamba watumishi wote wapatiwe mikataba inayoonesha kuwa wanatakiwa kufanya kazi kwa saa nane tu kwa siku. Ikiwa mfanyakazi atafanya kazi kwa saa zaidi ya nane basi atapatiwa nyongeza ya fedha katika mshahara wake kwa saa alizozidisha kwa kadri itakavyokuwa imepangwa na mwajiri wake. Pia kupitia nadharia hii kulipendekezwa kuanzishwa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo itatumiwa na wafanyakazi kuwekewa akiba ambayo itawasaidia mara baada ya kustaafu kufanya kazi (Wamitila, 2002).

Kimsingi, tunapoyatazama maelezo tuliyoyatoa hapo juu tunabaini kuwa nadharia ya Sosholojia ni nadharia inayohusu masuala ya kijamii. Methali ni moja kati ya kijitanzu cha fasihi ambacho kina uhusiano wa moja kwa moja na jamii. Masuala mengi kama si yote kati ya yale yanayozungumziwa katika methali yanatokana na mwingiliano wa jamii katika shunguli zake za kila siku. Methali huzungumzia

masuala yayohusu malezi, ndoa, kazi, kilimo, uvuvi, ufugaji, matambiko, mila na desturi, matatizo katika kazi, umuhimu wa maisha, kuheshimiana, kupendana, kujaliana, kuthaminiana, kuonya, kuadili na kuelimisha jamii mambo mazuri yahusuyo maisha. Mambo haya yote yanahusu jamii na hivyo kutumia nadharia ya Sosholojia katika kutafiti methali ni sahihi. Nadharia hii ya Sosholojia, tumeitumia katika kuchambua data zinazohusiana na dhamira katika methali za jamii ya Wasimbiti. Nadharia nyingine iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Simiotiki.

### 2.5.2 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni moja kati ya nadharia maarufu inayotumika katika kuchambua data za utafiti unaohusiana na muundo wa lugha pamoja na fasihi. Nadharia hii inatokana na nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdnand Dessaussure katika miaka ya mwanzoni mwa 1960 na kuwekewa misingi na wataalamu mbalimbali akiwemo Noam Chomsiky (Mark, 1995). Nadharia hii inahusika katika kuchunguza lugha ya ishara, picha, mafumbo na taswira inayojengwa katika kazi za fasihi kwa lengo la kuwasilisha dhamira kwa jamii iliyolengwa. Inaelezwa kuwa katika lugha huwa kunakuwa na vitu viwili ambavyo ni kitaja na kitajwa. Kitaja ni jina linalotaja kitu, mtu, mnyama au hali fulani, kwa mfano, Saidi, John, Mwajuma na Happyness ni majina ya watu. Majina ya wanyama ni kama vile mbwa, paka, simba, na tembo. Kitajwa ni umbo ambalo ndilo limetajwa na kitaja. Katika taaluma ya nadharia hii ya Simiotiki inaelezwa kwamba huwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kirejelee bali uhusiano uliopo ni wa dhahania tu (Eco, 1976). Hii inatokana na ukweli kwamba matumizi ya lugha ni ya kubuni ili kuwawezesha wanajamii kuweza kuwasiliana na kupashana habari na jumbe mbalimbali.

Matumizi ya lugha katika kazi za fasihi hutumia lugha ya ishara, picha, taswira na mafumbo ambayo ni ya kiishara zaidi kwa maana kwamba kinachosemwa huenda kikawa sio kile ambacho kimeandikwa bali kitu kingine kabisa (Ntarangwi, 2004). Upo uwezekano mtunzi wa kazi ya fasihi akawa anaelezea kuhusu fisi na matendo yake lakini kumbe anayezungumzwa pale ni mwanadamu mwenye sifa kama za fisi. Bila shaka mwanadamu huyo atakuwa ni mtu mlafi ambaye hawajali watu wengine bali hujali tumbo lake tu na familia yake. Matumizi ya lugha ya namna hii ni vigumu dhamira zake kuweza kueleweka kwa wasomaji au wasikilizaji kama itakuwa hawana ujuzi na maarifa ya nadharia ya Simiotiki.

Nadharia ya Simiotiki imeundwa katika misimbo ya aina tano ambapo ni kutokana na ujuzi wa maarifa ya misimbo hii ndipo msomaji anaweza kuipata vizuri dhamira iliyokusudiwa. Misimbo hiyo ni msimbo wa Kihemenitiki, Kiseme, Kiurejelezi, Kimatukio na Kiutamaduni (Barthes, 1994). Baadhi ya watunzi wa kazi za fasihi ikiwemo mashairi hutunga mashairi yao kwa kutumia misimbo hii kwa kujua na wakati mwingine bila hata kujijua. Katika utafiti wetu tumetumia misimbo yote hii katika kufanya uchambuzi wa data.

Msimbo wa Kihemenitiki hujitokeza katika matumizi ya lugha kupitia anuani ya kifasihi kama vile jina la kitabu, jina la shairi; wimbo na utenzi, jina onyesho katika tamthiliya na maigizo, jina la sura katika riwaya na hadithi na kadhalika (Nazarova, 1996). Baadhi ya dhamira katika kazi ya fasihi huweza kupatikana moja kwa moja kutoka katika jina la kazi hiyo hata bila msomaji kusoma na kumaliza kazi iliyowasilishwa mbele yake. Kupitia msimbo huu tutaweza kupata dhamira za kisiasa

katika mashairi ya magazetini kwa urahisi na tutakaposoma shairi zima ndipo tutathibitisha dhamira hizo. Hivyo, kwa kutumia mbinu ya usomaji makini tutakayoitumia katika kuchambua data za utafiti huu tutahakikisha kuwa tunasoma kwa makini methali zilizokusanywa ili kuweza kupata dhima zinazojengwa na mbinu za kisanaa katika methali za jamii ya Wasimbiti.

Msimbo mwingine unaounda nadharia ya Simiotiki ni msimbo wa Kiseme ambao unatokana na Semantiki yaani tawi la isimu linaloshughulikia maana ya maneno katika lugha (Mark, 1995). Katika kazi za fasihi ikiwemo mashairi wapo watunzi ambao hutumia maneno fulani na kurejelea maana hiyo tofauti na ile ya kisemantiki. Kwa mfano, mtunzi anaweza akatumia neno “buzi” kurejelea mtu ambaye hutoa pesa zake kwa wanawake wa nje ambao hufahamika kama vimada. Lakini maana ya kisemantiki ya neno hili hurejelea mnyama mbuzi ambaye katika hali ya kawaida anaweza kuwa ni mkubwa kuliko wengine ndio maana anaitwa buzi. Sasa ili msomaji aweze kuelewa kile kilichosemwa kifasihi kupitia neno hilo ni lazima awe na uelewa wa maana ya kisemantiki ya neno hilo. Katika utafiti wetu tutautumia msimbo huu wa kimatukio katika kuchambua dhamira zinazopatikana katika methali za jamii ya Wasimbiti wa Rorya mkoani Mara.

Aina nyingine ya msimbo ni ule wa Kiurejelezi ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kutumia mnyama kumrejelea mwanadamu (Ntarangwi, 2004). Kwa mfano, simba ni mnyama anayefahamika kuwa ni mnyama mkali sana na anaogopwa si tu na wanyama wengine bali wanadamu pia humuogopa. Katika maandishi mbalimbali, mnyama simba hutajwa kuwa ni mfalme wa mwituni kutokana na ukali wake. Katika

ulimwengu wa fasihi ya Kiswahili si jambo la ajabu kuona watunzi wakitumia mnyama simba kumrejelea mwanadamu ambaye anasadikika kuwa na sifa ya ukali kama wa simba. Kwa mfano, utaona katika kazi za fasihi kukiwa na sitiari kama vile, “Sufiani ni simba.” Hii ni sitiari inayoashiria kuwa huyo bwana Sufiani ni mtu mkorofi, mkali, asiye na huruma na haogopi kitu. Haya ni matumizi ya lugha ya kiurejelezi na huweza kuchambuliwa vizuri kwa kutumia msimbo wa kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki.

Msimbo wa kimatukio nao pia ni moja kati ya misimbo maarufu unaounda nadharia ya Simiotiki (Barthes, 1994). Msimbo huu hutumika kwa mtunzi kuunda matukio kimsimbo na kiishara katika kazi yake ya fasihi kama vile mashairi. Kwa mfano, mtunzi anaweza kutunga kisa chenye tukio linalofanywa na wanyama kama vile sungura na fisi. Matukio yanayofanywa na wanyama hawa katika hadithi mbalimbali za kimapokeo ni matukio yenye kusawiri maisha halisi ya jamii. Sungura ni mnyama anayesawiriwa kuwa ni kiumbe mwenye ujanja mwingi wa kuweza kumfanya apate kila kitu ambacho anakihitaji bila wasiwasi. Fisi ni mnyama anayesawiriwa kuwa ni kiumbe ambaye ni mjinga na anaweza kudanganywa kiurahisi. Katika hali ya maisha ya kila siku ya jamii wapo wanadamu wenye sifa kama hizi ambapo matukio ya fisi na sungura yanawagusa. Hivyo, katika kuchambua data za utafiti ni wajibu wetu kuwa makini katika kuchunguza matukio yanayowasilishwa mbele yetu kupitia methali za Kisimbiti ili tuweze kupata dhamira katika mashairi ya methali hizo.

Msimbo wa mwisho katika mtiririko wetu ni msimbo wa Kiutamaduni ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi hujenga dhamira kutokana na viashiria vya kiutamaduni

(Mark, 1995). Kwa mfano, katika jamii ya Wamakonde au kama wanavyofahamika kwa jina jingine la Wamakua huwa wana utamaduni wa kuwaweka ndani wasichana waliovunja ungo na kuwafundisha namna wanavyotakiwa kuishi na wanaume wao. Tukio hilo la kuwekwa ndani huenda sambamba na kuimba nyimbo na kucheza ngoma mara baada ya mafunzo kukamilika. Katika nyimbo na ngoma hizo kunaelezwa masuala ya kiutamaduni yanayohusiana na chakula, mavazi, malazi, mahusiano ya mume na mke na kuhusu heshima kwa watu wakubwa. Hivyo, katika kuchambua mashairi kama hayo inampasa mchambuzi kuwa makini na matumizi ya viashiria vya kiutamaduni katika mashairi hayo kwani ni katika viashiria hivyo ndipo dhamira zinapowasilishwa.

Katika utafiti wetu huu tutaitumia nadharia ya Simiotiki na misimbo yake yote mitano katika kuchambua data za utafiti huu. Data za utafiti zinazohusiana na matumizi ya mbinu za kisanaa katika methali za jamii ya Wasimbiti zitachambuliwa kwa kutumia nadharia ya Simiotiki. Hii ni nadharia muafaka kwa kuchambua data za aina hii kwani methali hutumia lugha ya picha, ishara, taswira na mafumbo katika kuelezea masuala tofautitofauti.

## 2.6 Pengo la Maarifa

Katika sura hii tumepitia kazi tangulizi mbalimbali lakini hatukufanikiwa kukutana na kazi hata moja ambayo imechunguza methali za jamii ya Kisimbiti. Methali za jamii ya Wasimbiti kama ilivyo kwa methali za jamii nyingine duniani zina mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii na hivyo zinahitaji kutafitiwa na kuhifadhiwa vizuri katika maandishi ili zitumike kwa vizazi na vizazi. Kwa kulitambua hili

tukaona kuwa ipo haja ya msingi ya kufanya utafiti huu ili kuziba pengo hili la maarifa.

## 2.7 Hitimisho

Hii ni sura ya pili ya utafiti wetu ambayo ilikuwa na lengo la kuwasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Katika sura hii tumefanikiwa kuwasilisha kazi tangulizi zinazohusiana na dhana ya methali, utafiti tangulizi wa methali duniani, matumizi ya fani katika methali, methali za makabila ya Tanzania na mkabala wa kinadharia; nadharia ya Sosholojia na nadharia ya Simiotiki. Sura inayofuata inawasilisha mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha vipengele mbalimbali vya mbinu za utafiti ambavyo vimesaidia katika kukusanya na kuchambua data. Vipengele vilivyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanyia data, mbinu za uchambuzi wa data, usahihi wa data na maadili ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti huhusisha mahali pa kijiografia ambapo ndipo data za utafiti zilipokusanyiwa kwa kuzingatia mbinu za ukusanyaji wa data zilizoelezwa katika sura ya tatu ya tasinifu hii (Kothari, 2008). Eneo la utafiti huu ni kata ya Komuge iliyoko katika wilaya ya Rorya kupitia vijiji vya Kyabhaibi, Kinesi, Iryenyi na Songambele. Vijiji hivi viliteuliwa kwa sababu ndipo mahali ambapo wanapatikana Wasimbiti wengi na hivyo kuwa na uhakika wa kupata data ambazo tulikuwa tunazihitaji. Katika vijiji hivi wapo wazee ambao walitoa mchango mkubwa wa kutuwezesha sisi kupata methali za Kisimbiti ambazo kwa sasa hazitumiki sana kutokana na mwingiliano wa jamii mbalimbali na pia mitaala inayotumika mashuleni inaruhusu ufundishaji wa methali za Kiswahili tu na sio zile za makabila.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni maelezo yanayotoa picha kamili juu ya namna utafiti ulivyotakiwa kufanyika tangu katika kukusanya data mpaka kukamilika kwa zoezi la

uchambuzi wa data (Robson, 2007). Kwa maneno mengine ni sawa na kusema kuwa usanifu wa utafiti ni ramani inayoelekeza namna utafiti husika ulivyofanyika. Utafiti huu niwa kimaelezo ambapo data za utafiti zimekusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia maelezo na si idadi au mkabala wa kimahesabu. Usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani yaani *Case Study*. Uchunguzi kifani ni usanifu wa utafiti ambapo mtafiti huteua mahali malumu ambapo ndipo panaweza kumpatia data za utafiti wake (Creswell, 2000). Mbinu hii ya usanifu wa utafiti ni nzuri kwa sababu humwezesha mtafiti kukusanya data za uhakika kwa sababu mahali ambapo amepachagua ndipo panaweza kumpatia data hizo. Pia, mbinu hii humwezesha mtafiti kukusanya data nyingi kwa kutumia muda mfupi na kufanikisha kazi yake. Hii ni kutokana na hali halisi kwamba hawezi kutumia  muda wake vibaya kwa kwenda sehemu nyingine ambayo haiwezi kumpatia data anazozihitaji. Kata ya Komuge ndiyo iliyoteuliwa kuwa ndio uchunguzi kifani wa  utafiti huu. Katika kata hii tulikusanya data katika vijiji vya Kyabhaibi, Kinesi, Iryenyi na Songambele. Usanifu huu wa utafiti umetusaidia katika kukusanya data za utafiti tulizozihitaji na kufanikisha utafiti wetu.

## 3.4 Kundi Lengwa

Katika utafiti wowote ule huwa kunakuwa na walengwa wa utafiti huo (Babbie, 1999). Walengwa katika utafiti huu walikuwa ni wazee wanaopatikana katika kata ya Komuge kupitia vijiji vinne vilivyoteuliwa. Wazee hawa ni wale wenye umri wa miaka 60 mpaka miaka 100 ambao bado wanaweza kuongea kwa ufasaha kwa msingi huu wale wenye uwezo wa kututajia methali tulizowaomba watutajie. Kundi lengwa hili liliteuliwa kwa sababu ndilo bado linafahamu vizuri methali za Kisimbiti pamoja na kufafanua mafunzo yanayopatikana katika methali hizo.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni wateule wachache kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa wanaopatikana katika kundi lengwa (Yin, 1994). Katika hali ya kawaida hakuna utafiti ambao unaweza kufanyika kwa kushirikisha kundi lengwa lote kwa mara moja na utafiti huo ukamalizika kwa muda mfupi. Pengine labda kama utafiti huo utachukua miaka mingi unaweza ukahusisha kundi lengwa lote la utafiti husika (Young, 1984). Kwa kulitambua hilo ndio maana katika utafiti huu tuliamua kuwa na sampuli ya Wazee 32 ambapo kulikuwa na wanaume 16 na wanawake 16 ikiwa ni 4 kwa kila kijiji. Watafitiwa 4 kwa kila kijiji ina maana kwamba wanaume walikuwa 2 na wanawake 2 kwa kila kijiji. Kwa kuwa jumla ya vijiji ilikuwa ni 4 ndipo sasa tunaweza kupata jumla ya watafitiwa 32 katika utafiti wetu.

Watafitiwa hawa walipatikana kutokana na kutumia mbinu ya usampulishaji tajwa. Usampulishaji ni kitendo cha kuteua watafitiwa kutoka katika kundi kubwa ili kupata wawakilishi wa kundi zima. Usampulishaji tajwa ni mbinu ya usampulishaji ambapo mtafiti huteua sampuli ya utafiti wake kwa kutajiwa na baadhi ya hao hao watafitiwa wake watu wengine ambao wanaweza kuwa sampuli ya utafiti huo (Robson, 2007).

Baada ya mtafiti kumpata mzee mmoja anayejua methali za Kisimbiti alifanya naye mahojiano na kupatiwa methali kadhaa za Kisimbiti. Mtafiti alimtaka mtafitiwa huyo amtajie mtafitiwa mwingine ambaye naye ni mjuzi wa methali za Kisimbiti na hali ikawa hivyo mpaka wazee 32 wakatimia. Mbinu hii ya usampulishaji ni nzuri kwa sababu humwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri kwa sababu huenda moja kwa moja kwa mtafitiwa aliyeelekezwa kwake na hatimaye kupatiwa data

anazozihitaji (Creswell, 2000). Kutokana na matumzi ya mbinu hii ya usampulishaji tuliweza kukusanya methali tulizohitaji katika jamii ya Wasimbiti na kuzifanyia kazi.

## 3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti huu ulikusanya data za upili na msingi kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata hapa chini.

### 3.6.1 Data za Msingi

Kama kichwa hiki kinavyosomeka, data za msingi ni kitu cha mwanzo kabisa kufanyika kabla ya mambo mengine yote. Data za msingi ni aina ya data za utafiti ambazo ndio zinakusanywa kwa mara ya kwanza kwa minajili ya utafiti (Babbei, 1999). Data za aina hii hazikuwahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa malengo kama haya ya utafiti huu. Katika utafiti huu, data za msingi zilikusanywa kutoka katika kata ya Komuge kupitia vijiji 4 vilivyoteuliwa na kuainishwa katika eneo la utafiti. Data za Msingi zilizokusanywa ni methali za jamii ya Wasimbiti pamoja na maelezo kuhusu methali hizo kutoka kwa baadhi ya watafitiwa.

### 3.6.2 Data za Upili

Utafiti huu pia ulikusanya data za upili na kama zinavyoitwa ni data ambazo tayari zilikwisha kukusanywa na watafiti watangulizi na kuhifadhiwa katika maktaba (Kothari, 2008). Data za upili hukusanywa kwa lengo la kujaziliza maarifa yanayotokana na data za msingi. Data za aina hii katika utafiti wetu zilikusanywa kutoka katika makala, tasinifu, wavuti, tovuti, vitabu, magazeti na machapisho ya vipeperushi vinavyohusiana na mada ya utafiti. Maktaba zilizotumika katika kukusanya data hizi ni maktaba ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Maktaba ya

Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Data za upili zilizokusanywa ni zile ambazo zinahusiana na mada ya utafiti wetu kutoka katika machapisho mbalimbali. Data hizi zilikusanywa ili kushadadia hoja zilizotokana na data za msingi.

## 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili na upitiaji wa nyaraka.

### 3.7.1 Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanya data za msingi kwa kufanya mahojiano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na watafitiwa wake (Kombo na Tromph, 2006). Katika kuitumia mbinu hii mtafiti hutakiwa kuandaa orodha ya maswali ambayo yatamuongoza katika mahojiano atakayofanya na watafitiwa wake. Maswali hayo ni lazima yaendane na malengo mahususi ya utafiti wake. Mtafiti aliitumia mbinu hii kukusanya data kutoka kwa wazee 32 ambao ndio sampuli ya utafiti huu. Kila mtafitiwa alitakiwa kutaja methali za Kisimbiti anazozifahamu na kila anapoitaja methali fulani alitakiwa kuelezea dhima ya methali hiyo. Zoezi la mahojiano lilifanyika mpaka pale watafitiwa wote walipotembelewa na kusailiwa. Mbinu ya usaili huru ndiyo iliyotumika katika kukusanya data za utafiti huu ambapo watafitiwa walipata uhuru wa kueleza yale tuliyowauliza bila mipaka. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya data za kutosha kwa sababu ni mbinu rahisi kukusanya data kwa watu ambao hawajui kusoma na kuandika. Watafitiwa karibu wote wa utafiti huu hawajui kusoma na kuandika lakini kuzungumza wanajua na hivyo tukaweza kukusanya data za kutosha kabisa kutimiza malengo ya utafiti wetu.

### 3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kusoma kazi tangulizi zinazohusiana na mada yake ya utafiti. Data za upili hukusanywa kwa lengo la kushadadia hoja zinazoibuliwa na data za msingi ili kuufanya utafiti kuwa ni wa kitaaluma zaidi. Katika kukusanya data za upili tuingia katika maktaba tajwa hapo juu na kutafuta kazi tangulizi ambazo zinazohusiana na mada ya utafiti wetu na kisha kukaa kitako na kusoma kazi moja baada ya nyingine. Katika kupitia kazi hizo tulihakikisha kwamba tumedondoa kila data ambayo tulidhani kuwa itatufaa katika utafiti wetu katika shajara maalumu tuliloliandaa likiwa na mungozo wa data tulizozihitaji. Kimsingi, kwa kutumia mbinu hii tuliweza kukusanya data za upili za kutosha na kusaidia kukamilisha malengo ya utafiti huu.

## 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kipengele muhimu ambacho kinawezesha data za utafiti kuchambuliwa na kupata matokeo ya utafiti. Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo.

### 3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data za utafiti unaohusiana na fasihi kama ulivyo utafiti huu. Mkabala huu kama unavyosomeka ni mbinu ya kuchambulia data za utafiti kwa mtafiti kutolea maelezo data alizozikusanya kwa namna ambayo inasaidia kujibu malengo mahususi ya utafiti wake (Kombo na Tromph, 2006). Data za utafiti huu zimewasilishwa kwa kutumia njia ya madondoo ambapo methali husika imedondolewa na kisha kufanyiwa uchambuzi kwa njia ya maelezo. Mbinu

hii ni nzuri na imewezesha kukamilika kwa malengo ya utafiti huu ambapo maelezo yaliyotolewa kuhusu data za utafiti yamekuwa yakishadidiwa na hoja kutoka katika kazi tangulizi na nadharia za Simiotiki na Sosholojia.

## 3.9 Usahihi wa Data za Utafiti

Usahihi wa data ni ile hali ambayo inafanya data za utafiti kuaminika kwa wasomaji wa kazi hii pale watakapokuwa wanaisoma kwa malengo tofautitofauti. Usahihi wa data za utafiti huu unatokana na mbinu zilizotumika katika kukusanya data kuwa ni mbinu muafaka na zimeteuliwa kwa umakini na ustadi wa hali ya juu. Sambamba na hilo pia uteuzi wa sampuli ya utafiti pia imefanywa kitaalamu kwa kuteua watafitiwa ambao wameweza kutoa data sahihi kwa minajili ya malengo ya utafiti huu. Pia, mtafiti amekuwa akipata maelekezo kutoka kwa msimamizi wake mara kwa mara katika kila hatua ya utafiti mpaka kumalizika kwake. Hivyo, kwa kufuata taratibu zote hizi tunaamini kuwa data tulizokusanya ni sahihi na zimetimiza malengo ya utafiti wetu.

## 3.10 Maadili ya Utafiti

Maadili ni miiko ambayo inatakiwa kuzingatiwa pale mtu anapofanya jambo fulani. Maadili ya utafiti ni dhana inayorejelea taratibu na kanuni ambazo mtafiti anatakiwa kuzingatia katika hatua zote za utafiti wake. Miongoni mwa maadili ya utafiti ni pamoja na kutunza siri za watafitiwa, kutolazimisha watafitiwa ambao hawataki kuhojiwa wahojiwe kwa lazima na kuweka kumbukumbu sahihi kama vile zilivyoelezwa na watafitiwa. Maadili yote haya yalizingatiwa katika utafiti huu ili kufanya matokeo ya utafiti kuwa ni sahihi na yenye kuaminika.

## 3.11 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza vipengele mbalimbali vinavyohusiana naukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti kwa lengo la kuwezesha kukamilika kwa malengo ya utafiti huu. Vipengele tulivyoviwasilisha katika sura hii ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa; data za msingi na data za upili. Vipengele vingine ni mbinu za kukusanya data; usaili na upitiaji wa nyaraka, mbinu ya kuchambua data; mkabala wa kimaelezo, usahihi wa data na maadili ya utafiti. Sura inayofuata imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti hufanywa ili kuufanya utafiti ufikie malengo yake. Kothari (2008) anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kupanga, kuhakiki, kulinganisha, kutofautisha data za utafiti na kuzitolea maelezo kwa namna ambayo inasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Katika utafiti huu data za utafiti zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kuongozwa na nadharia za Sosholojia na Simiotiki. Ili kuufanya uchambuzi wa data za utafiti huu kuwa fanisi tuliamua kuchambua data za utafiti kulingana na malengo mahususi ya utafiti huu. Malengo hayo mahususi yalikuwa ni kubainisha dhima ya methali za jamii ya Wasimbiti wa wilaya ya Rorya mkoani Mara, kuelezea uhalisia wa dhima za methali za jamii ya Wasimbiti kwa jamii ya leo na kufafanua mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga methali za jamii ya Wasimbiti wa wilayani Rorya mkoani Mara. Lengo mahususi la kwanza na la pili yana ufanano wa kimantiki na hivyo tumeyaunganisha malengo hayo katika uchambuzi wa data. Data za utafiti za malengo haya matatu zimewasilishwa na kuchambuliwa kama ifuatavyo:

## 4.2 Dhima ya Methali za Kisimbiti

Methali za Kisimbiti kama zilivyo methali za jamii nyingine duniani zina dhima tofautitofauti kwa jamii hiyo. Tunapozungumza juu ya dhima ya methali tuna maana kuwa methali hizo zinatumiwa au zipo katika jamii kwa ajili ya kufanya nini, nini kazi ya methali hizo? Majibu ya maswali haya ndiyo hutupatia dhima za methali hizo

ambazo mfano ni, kuonya kukosoa, kutahadharisha, kutoa maonyo juu ya matendo mabaya, kuelimisha, kuhimiza kufanya kazi kwa juhudi, kuachana na tama, kukubali mabadiliko, kutenda haki na kuonesha umoja na mshikamano.

Dhumuni mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza dhima ya methali za Kisimbiti wa wilaya ya Rorya mkoani Mara. Dhumuni mahususi la pili lilihusu kuelezea uhalisia wa dhima za methali za jamii ya Wasimbiti wa wilayani Rorya mkoani Mara. Dhumuni la tatu ni kuelezea mbinu za kisanaa zilizotumika kujenga dhima za methali za jamii ya Wasimbiti.Uwasilishaji wa data umefanywa kwa kuandika methali ya Kisimbiti, kuitolea tarjama au tafsiri ya Kiswahili na kisha kuandika dhima yake. Mwishoni mwa kila data tumefanya uchambuzi kwa muhtasari juu ya data hizo. Kwa kuwa si rahisi kuchambua methali zote zinazozungumzia dhima fulani kwa maelezo marefu tumeamua kuwasilisha kwa mfumo huo tulioueleza na kisha kutoa uchambuzi wa kimajumuisho kwa kila dhima. Ufuatao ni uwasilishaji wa dhima za methali za jamii hiyo:

### 4.2.1 Kuacha Tamaa na kuwa na Subira

Kuwa na tamaa ni kule kuwa na uhitaji wa kitu ambacho mtu hana uwezo nacho kwa wakati ambao hawezi kukipata. Kuwa na subira ni kusubiri kitu ambacho mhitaji anatarajia kukipata kipindi ambacho hitaji hilo halijawa tayari au hakuna uwezo wa kukipata kwa wakati huo, lengo ni kumwelekeza mtu akubali kutumia mali kidogo kidogo kwa utaratibu mzuri mpaka itakapokuwa nyingi. Methali mbalimbali zimeonesha kubeba dhima ya kuwaasa wanajamii wa Kisimbiti kuepukana na tamaa ya kupata vitu ambavyo ni vya hali ya juu kulingana na uwezo wao.

Methali hizo ni hizi zifuatazo:

1. **Methali:** ***Nyilandulya yatondaini no nyakolokotwi***

Tar- jama: Mwendapole alipambana na mwenye nguvu

Maana: Ni bora ya kuwa na mtu anayefanyakazi kwa utaratibu na kazi inaonekana kuwa nzuri, kuliko kuwa na mtu anayefanya kazi kwa papara na kuharibu kazi napengine kutomaliza kabisa.

Dhima: Kutuasa kuwa kutokuwa na papara katika kazi kwani waweza kuharibu kazi, ni bora kufanya kazi taratibu na kwa umakini na kazi ikawa nzuri na yakupendeza.

2. **Methali:** ***Mosemya yaakërrë M öröösnia***

Tarajama: Kujiandaa ni bora kuliko kukurupuka kufanya jambo bila mipango.

Maana: Ni vema kufanya mipango yako kwa kujianda katika maisha,Kuliko kukurupuka katika jambo lolote kwani waweze kuleta matatizo.

Dhima: Kuwa makini katika maisha yetu, kutokurupukia tusiyoyajua na hatimaye yaweza kuhatarisha maisha yatu.

3. **Methali:** ***Nyakemamaana yaarëëyë beno batehëëyë***

Tar-jama: Mlafi (mwenye uchu wa chakula) alikula chakula kisichoiva.

Maana: Mwenye tamaa ya kupata yote kwa pupa huishia kukosa yote au kupata hasara, kwani hushindwa kukabiliana na vikwazo.

Dhima: Kuwa na subira katika maisha na kutokuwa na tamaa ya kupata vyote kwa pupa.

4. **Methali:** ***Obha na itamwe otabha bosahe.***

Tar – jama: Heri kuwa na mwana tahira kuliko kukoswa kabisa.

Maana: Heri kufanikiwa kupata kidogo hatakama sikamili kuliko kukosa kabisa. Au ni bora kuzidiwa na mengi ya kufanya kuliko kungoja kukosa cha kufanya.

Dhima: Hutumiwa kwa mtu mwenye tamaa anayeacha kidogo kwa kutegemea kingi.

5. **Methali:** ***Ghenda ng'ora uhike hano ukuya!***

Tar- jama: Nenda polepole ufike unako kwenda

Maana: Inafaa kutenda mambo kwa mpango na kwa kufuata utaratibu, pupa itakukuharibia mafanikio.

Dhima: Hutumika kwa watu wanaofanya papara katika shughuli zao mwisho wao hudhurika au huishia kupata hasara; Ni vyema kufanya kila kitu kwa kufuata mpango mzuri na kwa utaratibu.

6. **Methali:** ***Eng'ora yahire obosara mokerandi***

Tar- jama: Taratibu taratibu iliingiza togwa kibuyuni.

Maana: Bora kufanya mambo kwa utaratibu na kwa mpango, kuliko kuharakisha na kuharibu.

Dhima: Kutokuwa na pupa katika maisha.

7. **Methali:** ***Mokambi wa bhoke takokomba kamwehe;***

Tar -jama: Mchovya asali hachovi mara moja

Maana: Mtu yeyote aliyekwisha kutambua faida au uhondo wa jambo fulani hakomi kufanya tena na tena au mtu akishatambua manufaa ya jambo basi hutafuta namna ya kupata zaidi Ili aweze kufaidi zaidi.

Dhima: Hutumika katika kuonya watu wenye tamaa ya kutoridhika na kile walichopata au kilewalicho nacho na kupenda kupata zaidi na zaidi (kuacha tamaa ya kujilimbikizia mali).

8. **Methali:** ***Nyakemamano yaleye amakayelya (bhetaheye).***

Tar- jama: Mrafi/mwenyepupa alikula vilivyo vibichi.

Maana: Mwenye tamaa yakupata kila akionacho huishia kukosa yote kwani hushindwa kujipanga vema kukabiliana na vikwazo au magumu yaambatanayo navyo.

Dhima: Kuwa mvumilivu na subira kwani kufanya jambo kwa pupa ama bila mpangilio huishia kuharibu au hata kujidhuru mwenyewe.

9. **Methali:** ***Emboseri iyo omokangi nu Butindi.***

Tar – jama: Ari ya mjinga ni jeuri

Maana: Ujeuri wa mjinga kutaka kupinga anachoshauriwa ndio unaomwongoza kufanya jambo.

Dhima: Kukubali kushauriwa na kukubali mabadiliko.

10. **Methali:** ***Ono atana enonkwe takunyora nonkwe yendehë.***

Tar- jama: Asiye na bahati habahatiki.

Maana: Iwapo huna bahati ya kupata kitu fulani basi hutakipata hata ukijaribu kukitafuta kwa juhudi namna gani.

Dhima: Hutumiwa kwa mtu anayejaribukutafuta mambo mengi bila kufanikiwa.

11. **Methali:** ***Enonko iyowonde, utakatigha ekoseku kya samereyehë***

Tar-jama: Bahati ya mwenzio usiache mlango wazi.

Maana: Usidhani unaweza kuiga mambo yote na kutumia mbinu zaidi ili kupata bahati aliyonayo mwingine.

Dhima: Hutumiwa kwa mtu ambaye anatumaini kwamba atafanikiwa kutokana na fanaka za watu wengine.

12. **Methali:** ***Ekekere nkehashire amanshe, kasi ta manshe gho morohë***

Tar-jama: Chura hupenda maji lakini si maji ya moto

Maana: Ingawa mtu hupenda jambo si vizuri kupenda kupindukia

Dhima: Huonya wale wanaopenda vitu fulani na kuwa na hamu yake sana kwani vinaweza kuwaletea madhara au vikawadhuru.

**13. Methali: *Omoremo ogwo lusiko lomwe toghoko hasha mughihë***

Tar-jama: Kazi ya siku moja haijengi nyumba

Maana: Usiwe na pupa kutaka matokeo ndani ya muda mfupi. Kuwa tayari kufanya kazi kwa juhudi na subira, utafanikiwa.

Dhima: Kuwa na subira, usiwe na pupa.

**14. Methali: *Kera kento nkena enkagha yaye***

Tar-jama: Kila jambo lina kipindi chake

Maana: Kila kitu kina muda wake mwafaka inafaa kifanywe au kitumike kwa muda muafaka.

Dhima: Ni vyema kufuata utaratibu wa kila jambo au muda unavyotakiwa kufanya usilazimishe jambo.

**15. Methali: *Imbura tetwe rero ubusu rero oghese rero – hë***

Tar-jama: Mvua hainyeshe leo upande na uvune leo .

Manaa: usifanye pupa kutegemea matokeo ya hapo kwa hapo, lipe jambo muda litoa matokeo mazuri baadae.

16. **Methali:** ***Endwe hano ekerwe ne nshara, nenyanki ekorya***

Tar-jama: Simba akizidiwa na njaa, hula majani

Manaa: Mtu akikosa chaguo lake hulazimika kuchukua kilichopo hata kama hakipendi.

Dhima: Hutumika kwa wale watu wanaopenda kung'ang'ania jambo moja tu bila kuwa na uchaguzi wa kitu kingine.

17. **Methali:** ***Eng'ana ne ng'ora Ikuya.***

Tar-jama: Subira ya vuta kheri

Maana: kutumika au kuwa tayari kusubiri mambo yanapokwenda vibaya, hutuletea faida au manufaa hapo baadaye.

Dhima: Kuwa na subira.

18. **Methali:** ***Enyako ya rero na mashomera gha isho.***

Tar-jama: Taabu ya leo ndiyo furaha ya kesho

Maana: Kuwa tayari kuvumilia magumu unayokutana nayo katika jitihada zako za kujenga maisha kwani msingi wa mafaniko ni jitihada zako.

Dhima: Kuvumilia taabu zote zinazoweza kutokea na kutafuta suluhisho.

19. **Methali:** ***Etemo twikwibhisahe, nokabhisa mungibho:***

Tar-jama: Tabia haifichiki hata ukificha katika nguo

Maana: Mwonekano mzuri wa mtu haufichi, kwani tabia,mwenendo hudhihirisha tabia yake.

Dhima: Hufichua wenye tabia ya unafiki na wanao ficha tabia zao mbaya.

Methali hizi kwa jumla wake zinazungumzia juu ya namna ambavyo binadamu anatakiwa kuwa ili kuhakikisha kwamba anaepukana na tamaa ya kutaka vitu ambavyo hana uwezo navyo. Katika maisha ya kila siku , mwanadamu hutamani vitu vizuri hasa vile ambavyo vitamfanya kuwa na maisha mazuri kama vile nyumba nzuri, gari, mke/mme mzuri na fedha nyingi kwa ajili ya matumizi. Wananadharia ya Sosholojia wanaeleza kuwa katika jamii hakuna mtu ambaye anapenda kuishi maisha ya shida wala taabu kwa sababu mbalimbali lakini kubwa ikiwa ni kwamba mwenye mali huthaminiwa na asiye nacho hudharauliwa (Turner, 1999). Hivyo, kila mtu hupenda kuthaminiwa na siyo kudharauliwa na kwa maana hiyo atafanya kila linalowezekana ili kuhakikisha kwamba anapata mali ili aweze kuthaminiwa.

Methali za jamii ya Kisimbiti zinakubaliana na maelezo kwamba kila binadamu anapenda kuheshimiwa na kuthaminiwa. Kwamba hiyo ndiyo saikolojia ya jamii na ya mtu mmojammoja. Hata hivyo methali hizo hizo zinapendekeza kwamba ni vizuri kwa wanajamii kuwa na subira na kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili siku moja waweze kufanikiwa kupata yale wanayohitaji. Methali hizi zinafanana na zile za Kiswahili zinazosema kuwa “subira yavuta heri, haraka haraka haina baraka na mwenda pole hajikwai. Methali namba 18 inathibitisha kwamba mtu anatakiwa kuwa mvumilivu katika maisha kwa kuridhika na kile anachokipata ili siku moja

aweze kufanikiwa. Ikiwa mtu ana tamaa na vitu vya watu anaweza kujiingiza katika maovu na hatimaye aishie kufungwa na kuyakosa yale yote aliyotaraji kuyapata. Mtafitiwa mmoja aliyetutajia methali hii anasema kuwa,

> *Watu wengi wa siku hizi hasa vijana wanapenda kuwa na maisha ya juu kuliko uwezo wao. Utaona baadhi yao wanajiingiza katika vitendo vya rushwa ili waweze kupata fedha ambazo si jasho lao kwa ajili ya kuwa na maisha ya anasa. Si jambo la ajabu kuona mtu ambaye ameanza kazi muda mfupi tu uliopita na tayari ameshapata maendeleo makubwa kama kuwa na nyumba, gari, kumiliki mashamba na viwanja na ukwasi wa ajabu kabisa. Utajiri wa namna hii ameupata wapi kama sio rushwa na ufisadi?*

Maelezo ya mtafitiwa huyu ni ya kweli kwani katika jamii ya leo kila mtu hutamani kuwa na maisha mazuri hata kama ni kwa kutumia njia ambazo si halali. Methali za Kisimbiti zina nafasi kubwa ya kuionya jamii ili iachane na tamaa na kufanya kazi kwa subira na uvumilivu. Methali zote hapo juu kuanzia namba 1 mpaka 18 zina uhalisia katika maisha ya leo. Jamii ikizitumia vizuri methali hizi itasaidia katika kujenga vijana wenye maadili na uzalendo katika kutumikia nafasi za utumishi walizopatiwa kwa manufaa ya jamii yao na taifa kwa jumla (Mulokozi, 1996).

Kimsingi, methali za jamii ya Wasimbiti zina dhima nyingi zenye uhalisia katika maisha ya jamii ya leo. Katika kuthibitisha hilo, dhima nyingine ya methali za jamii hiyo ni kuelimisha jamii kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata.

### 4.2.2 Kuelimisha Jamii

Kuelimisha jamii ni dhima ya methali za jamii karibu zote duniani (Sengo, 2009). Kama tulivyowahi kusema mahali fulani katika tasinifu hii ni kuwa moja kati ya dhima kubwa ya methali ni kutoa elimu kwa jamii. Kabla ya ujio wa wakoloni ambao walianzisha mfumo rasmi wa kutolea elimu, elimu ilikuwa ikitolewa kwa

kutumia methali na vipengele vingine vya fasihi simulizi. Hata hivyo, pamoja na wakoloni kuanzisha mfumo rasmi wa kutolea elimu lakini bado methali ziliendelea kufanya kazi hiyo kwani wanajamii wengi hawakupata nafasi ya kusoma katika shule mpya zilizoanzishwa na serikali ya kikoloni. Na hata kama wote wangeweza kupata nafasi ya kusoma katika shule hizo bado nafasi ya methali katika kuelimisha jamii inabaki pale pale. Methali ambazo zinaisawiri dhima ya kuelimisha jamii ni hizi zifuatazo:

20. **Methali:** ***Hano Omona Okoŕeye ekegheso, mohane.***

Tar- jama: Mtoto anapolilia kisu mpe, akijikata atakiacha mwenyewe.

Maana: Mwana mkaida akikataa makanyo/ maonyo, akidhani kuwa unamnyima jambo zuri basi mwache, litakapomdhuru atajifunza. Methali hii ni sawa na ile isemayo mtoto akililia wembe mpe.

Dhima: Kuwahimiza wazazi/walezi kuwalea watoto wao vyema kwa kuwaongoza vizuri.

21. **Methali:** ***Ekobhasha/Embasho eno erënge mubaasho iyho ekobhasha.***

Tar-jama: Tezo iliyondani ya seremala au aliyonayo seremala ndiyo inayotumika katika shughuli za uchongaji.

Maana: Tuthamini mali tulizonazo vyombo sasa kwani ndiyo inayotusaidia katika shughuli yoyote tuliyonanyo.

Dhima: Thamini ulichonacho leo.

22. **Methali:** ***Otakaasheengera Umunyeenye ugwa ömögondo, keno onakyo kyo ikyaho.***

Tar-jama: Furahia ulichokula na si shamba lipendezalo.

Maana: Hupaswi kujivunia/kuringia shamba linalopendeza machoni kwani mvua inaweza kukosekana na shamba lote likakauka kabisa, hivyo ni bora kujivunia kile ulichovuna na kile unachokula sasa.

Dhima: Thamini ulichonacho sasa mkononi kuliko kuthamini kilichoshambani au kwingineko ambapo hujui utapata au utapoteza kabisa.

23. **Methali:** ***Ona atana Omokaamoona, nu – mwene akwikamoonera.***

Tar-jama: Asiye na mkaa mwana, hujipikia/ hujihudumia mwenyewe.

Maana: Anayekosa chake binafsi hakosi kutaabika. Au kama huna chakwako Kitakachoweza kukufaa itabidi utafute namna ya kujiokoa kwani hakuna atakayekupa vya kwake. Au asiye na msaada wa kutatua shida zake hana budi kujitahidi kutatua mwenyewe.

Dhima: Kujiandaa katika maisha pindi unapokosa msaada basi uwe na msaada mwingine wa kukusaidia.

**24. Methali:** ***Umuhyo görëngë yeeka, te-gokobora moremohë***

Tar – jama: Shoka iliyo nyumbani haiwezi kukosa kazi

Maana: Kitu chochote ulichonacho hata kama ni dhaifu chaweza kukufaa katika kazi fulani na siku yoyote. Akiba hata iwe duni ipo siku itakufaa tu.

Dhima: Kuhimiza kuweka akiba kwa faida ya baadaye, kwani akiba hiyo kuna siku itakusaidia tu. Methali hii ni sawa na ile isemayo Akiba haiozi au Akiba si mbaya ingawa ya kumbi, siku ya vumbi hutia motoni.

**25. Methali:** ***NyambisaÖbarööyë,sekerro keremoboorä.***

Tar-jama: Mficha maradhi, kilio kitamuumbua.

Maana: Anayefanya siri matatizo yake huumbuka pale yanapomzidiamakumgharimu atakapoonekana.

Dhima: Hutumika kwa watu ambao hawataki kusema matatizo yao kwa kuona haya/aibu, hivyo ni vema kusema matatizo yako, kwani kwa kufanya hivyo, huweza kutatua shida zako napengine kupata msaada zaidi.

**26. Methali:** ***Hano enshansha etaho, nenkali ekoghogwa.***

Tar-jama: Kama hakuna mnyama dume, Jike ndilo huchinjwa.

Maana: Kilichopo ndicho kinachoweza kutumiwa/kutumika kuliko kung'ang'ania kisichokuwepo kwa wakati huo.

Dhima: Kuthamini tulivyonavyo sasa na kuvitumia pale panapohitajika.

**27. Methali:** ***Lyamotobhu twikwibwebwahe! Ni iyu mwamweikwubwebwa***

Tar- jama: Jambo lolote la maskini halisikiwi hata akizungumza ukweli,lakini tajiri hata akisema uongo hukubalika/ husikiwa.

Maana: Mara nyingi mwenye uwezo ndiye anayethaminiwa zaidi kuliko maskini asiyekuwa nacho.

Dhima: Kuthamini watu wote hata kama ni maskini kiasi gani,Watu wote wathaminiwe. Methali hii ni sawa na

Methali hii, *Aliyenacho ndiye aongezewaye – ono yanakyoalongelibwa. (Kisimbiti).*

**28. Methali:** ***Omughe ghonogolaye kebhara, toghokororahe.***

Tar-jama: Mshale uliolala nje, hauna makali tena

Maana: Yeyote anayekataa maonyo ya wazazi/walezi wake si mtotoaliye mwema ni mtukutu. Kumfunza adabu akiwa mdogo badoakikomaa hatafundishika tena.

Methali hii ni sawa na ile isemayo. Samaki mkunje angali mbichi

Dhima: Walezi na wazazi kudhibiti jambo mapema iwezekanavyo ili tatizo hilo lisije likakomaa na kushamiri hata likakushinda/au unapomwonya mtoto asikusikilize, mwache dunia itamwonesha. Methali hii inawaonya pia wazazi/ walezi walio katika familia zao, kushindwa kusimamia majukumu ya watoto wao/familia yao.

**29. Methali:** ***Ensaho Oyomoghaka, tekoheta bosahë***

Tar-jama: Furushi la mzee halikosi chochote

Maana: Mtu mzoefu, Aliyeishi miaka mingi aliyena maarifa, daima huwa na jema lakusema na huwa naMaarifa, daima huwa na jema la kuwafaa wengine.

Dhima: Kuwaheshimu na kuwathamini wahenga wetu na wale wanaotuzidi umri.

**30. Methali:** ***Insintwaraiisya mumighi, nsilighuita***

Tar-jama: Uhuni/utembezi wako wa kwenye miji utakuua:

Maana: Mke na mme wasio na waaminifu katika ndoa zao,Utembezi wao utawaletea kifo au majanga katika Familia zao.

Dhima: Uaminifu katika ndoa katika na familia zao.

**31. Methali:** ***Omotaka nomwene aimanyire:***

Tar- jama: Maskini/fukara,yatima,hujihudumia mwenyewe.

Maana: Kila mtu anayepata shida hujifahamu nafsi yake ilivyo hivyo hujihudumia mwenyewe kwa sababu hakuna atakayekusaidia kutatua matatizo yako.

Dhima: Kuwa imara katika kutatua matatizo hayo hasa kama wewe ni fukara

**32. Methali:** ***Wenyuwenyu hakabha haghogho wenyu tohangehë.***

Taar-jama: Kwenu ni kwenu hata kama ni pabaya ni kwenu.

Maana: Mtu huwezi kuringia maeneo yasiyo ya kwake kwani si kwenu, hivyothamini ulichonacho hata kama ni kibaya kwani ndicho chako.

Dhima: Kuthamini ulichonacho au mazingira na tamaduni ya kwenu, si kuthaminimitindo, tamaduni au chochote kisicho asili yako.

**33. Methali:** ***Mosani kubhane, kubhaho ntukuntunahe***

Tar – jama: Rafiki kwa vyangu kwa vyako si rafiki tena.

Maana: Mimi nipatapo kitu wewe unataka tukitumie sote lakini wewe Ukipata chako unajaitenga kabisa.

Dhima Hutumiwa kwa mtu anayependa kubania vitu vyake yeye mwenyewe na kutaka kutumia vya mwenzake hivyo kuacha uchoyo.

**34. Methali:** ***Mbhini wabho kutuhware!***

Tar – jama: Mcheza kwao hutunzwa

Maana: Anayewatendea ndugu au jamaa zake mambo mema hakosi kupata fadhilakutoka kwao.

Dhima: Kutenda mema/fadhila katika maisha.

**35. Methali:** ***Gheghaini Ibhere ghetakuikara ihisho imwehë***

Tar – jama: Fahari wawili hawawezi kukaa zizi moja

Maana: Watu wenye vipawa vyakufanana hawawezi kushirikiana kwani kila mmoja atajaribu kuonesha uwezo wake kumpiku mwenzake.

Dhima: Hutumiwa kwa watu wawili ambao wanashindana na wananguvu sawa.

**36. Methali:** ***Moghambi wa mbele ninting'ane no moghambi wa nyuma ni ting'ane ense***

Tar-jama: Msemaji wa mwanao ana sifa zake na yule wa pili ana sifa yake pia.

Maana: Anayetangulia kufanya jambo ana nafasi nzuri ya kufaidika kuliko anayekuja baadaye.

Dhima: Kuhimiza jamii kuwa na tabia ya kuwahi kutekeleza jambo kwa wakati.

**37. Methali:** ***Motobhu uwabho tarige mwame wameikoheë***

Tar- jama: Maskini kwao si tajiri kwa aliye nje

Maana: Mtu hawezi akathaminika akiwa kwao, lakini anapokuwa nje ya kwao anathaminiwa.

Dhima: Kuelimisha jamii kuthamini nyumbani kwenu/kitu ulichonacho.

**38. Methali:** ***Mughuru Kwo abhande waho kolale***

Tar- jano: Nguvu kwa mwingine wewe kwako kunalala.

Maana: Mtu anathamini kwingine kuliko kwake au kwao.

Dhima: Kuthamini nyumbani kwako zaidi kuliko kwingine

**39. Methali:** ***Omona Umwikari, akerenge moke***

Tar-jama: Mkalishe mtoto akingali mdogo.

Maana: Lengo ni kumwonya mtoto, tangu utoto wake, usisubiri baadae, atakushinda. Au mtoto mfunze adabu akiwa bado mdogo, akikomaa hawezi kufundishika.

Dhima: Kutolea mafunzo kwa walezi/wazazi na wanafunzi/ watoto kuwa na maadili mema.

**40. Methali:** ***Amang'ana amaiya, nyinko ghakomahekana.***

Tar – jama: Mambo mazuri huonekana asubuhi.

Maana: Uzuri wa jambo lolote hutambulika mapema hata kwa namna linavyoanza au mtu anapoambiwa ni mwema huonekana tangu akiwa utotoni.

Dhima: Kuhimiza jamii kuendeleza yaliyomazuri katika maisha yetu, na endapo watagundua kuwa ubaya wa jambo basi nikuliepuka.

**41. Methali:** ***Hano Unyore Inyako, nkunyorore eno ena esanga yako***

Tar- jama: Apatikanaye na mkasa hupatikana na kisa.

Maana: Mtu anapofikwa na jambo baya, wengi husema mengi juu yake.

Dhima: Tusiwe wepesi wa kuhukumu/ kusema jambo bila kuwa na ushahidi wa kutosha.

**42. Methali:** ***Ono atamanyire ensoko ntemontohë***

Tar – jama Asiyejua utu si mtu

Maana: Asiyethamini au kuwajali wengine basi hana thamani.

Dhima: Kuthamini na kuheshimu watu wengine

**43. Methali:** ***Ono atakwikerya okokerwa, temokerihë***

Tar – jama Asiyekubali kushindwa si mshindani

Maana: Mshindanaji anapaswa kujua kuwa anaweza kushinda ama kushindwa na anaposhindwa anapaswa kuelewa na kukubali ushindi huo.

**44. Methali:** ***Okosoribwa komwishokoro, korarwa haresokorowabo***

Tar- jama: Badiliko la mjukuu, huanza na babu yake.

Maana: Ili mtu au kitu kirekebishwe hatua za kukirekebishazapaswa zichukuliwekukingali bado kichanga au mapema, la sivyo kikikomaa hakitafaa kubadili tena.

Dhima: Hutumika kuwakumbusha wazazi/walezi kulea/kuwapa mafunzo mema watoto wao tangu udogo wao, kwani wakikomaa hawafundishiki tena.

**45. Methali:** ***Enshera entambe, tekobhora kwikonyahë***

Tar-jama Njia ndefu haikosi kuwa na kona au haikosi kujipinda.

Maana: Hakuna jambo lililo timilifu ama jambo zuri lisilo na kasoro hivyo usistaajabu. siku litapoonesha dosari, hivyo hivyo maisha hayakosi changamoto na matatizo.

Dhima: Hukumbusha jamii kuwa hakuna mtu au jamii yoyote isiyokuwa na kasoro.

**46. Methali:** ***Mokaho akabha muya, takabhora kiberahë***

Tar-jama: Mke mzuri, hakosi kilema

Maana: Hata jambo lionekane kuwa zuri na lenye manufaa halikosi kuwa nakasoro.

Dhima: Hutukumbusha na kujua kuwa hata ukiwa mzuri namna gani hukosi kuwa na kasoro hakuna

aliyekamilika katika maisha tuliyonayo/tunayoishi katika jamii zetu.

**47. Methali:** ***Ono abhombirwe takobhora busaryahë***

Tar – jama: Binadamu hakosi baya

Maana: Hakuna aliyekamili, kila mtu ana ubaya wake.

Dhima: Jamii itambue kuwa kila mtu ana kasoro zake.

**48. 49. Methali:** ***Ikyaho hano kigundirë tikikunyonkerahë!***

Tra- jama: Chako hata kikioza hakikunukii.

Maana: Jambo lako lolote linapokuharibikia au kwenda vibaya (hasa mwanao anapokuwa mtukutu) hupaswi kulitelekeza bali endelea kujitahidi kulitengeneza.

Dhima: Hutumika katika kuhimiza wazazi/walezi kujitahidi kulea watoto bilakukata tamaa hata kama ataendelea kuwa mtukutu.

**49. Methali:** ***Enda tinditohe kasi eakobörä***

Tar-jama: Chawa si mzito katika nguo yako lakini hukusumbua

Maana: Mtu aliye dhaifu au asiye na maarifa ukiishi naye si rahisi kukushinda au kukudhuru, lakini matendo au kauli zako zaweza kukuaibisha.

Dhima: kujihadhari na wale wanaoweza kukuaibisha au kuaibisha wengine

**50. Methali:** ***Tighana na amaghogho naghogonse gakotighe***

Tarjama: Epukana na maovu ili maovu nayo yakuepuke.

Maana: Jikinge na mambo maovu au mabaya ili ujiepushe na matatizo.

Dhima: Hutumika katika malezi hasa kuwaasa vijana na watoto kutotafuta matatizo, wasikilize wanayoambiwa au kushauriwa na wakubwa wao.

**51. Methali:** ***Amashomeroageekekondo, esesetekosaha momashomerwa gabohë***

Tar jama: Furaha ya tumbiri/ngedere, mbwa hashiriki.

Maana: Mtu yeyote hafurahii adui yake anapofanikiwa ama kufurahia kitu.

Dhima: Kuwaonya watu wanaoona wivu pale mwingine anapopata mafanikio.

**52. Methali:** ***Amashomero ghu mwibori nkoseka kya Mona***

Tarjama: Furaha ya mzazi, kicheko cha mwanae.

Maana: Mtu hufarijika/hufurahia mafanikio apatayo mtu anayempenda mathalani mwanaye.

Dhima: kutia faraja.

**53. Methali:** ***Oghoterwe ingibho otakaghoterwa no omotwe***

Tarjama: Ni heri uishiwe na nguo kuliko kuishiwa akili.

Maana: Ni heri kukosa uwezo wa kufanyakazi au kitu chochote kuliko kukosa matumaini katika maisha.

Dhima: Umuhimu wa Elimu katika maisha

**54. Methali:** ***Ikyaho nkerakotori***

Tarjama: Kimfaacho mtu ni kile kilicho chake.

Maana: Kinachoweza kukutatulia matatizo yako kwa uthabiti ni kile ulichonacho wala si kile cha kutegemea toka kwa mwingine.

Dhima: Thamini ulichonacho si kutegemea chamwenzio

**55. Methali:** ***Ukwikara na muhiri waho nkoremerya***

Tar – jama Kuishi na nduguyo kwataka subira

Maana: Ukiishi na nduguyo yakupasa uwe mvumilivu kwani zipo kero nyingi zinazoweza kujitokeza.

Dhima: Kuwa na uvumilivu katika kuishi na nduguyo.

**56. Methali:** ***Nyamoghamba kwebare, nyamobhorwa kuhitare***

Tar- jama: Mtoa matamshi husahau, mtamkiwa hukumbuka, au mtenda husahau, mtendewa hasahau.

Maana: Mtu husahau fadhila atendewazo ila atendaye fadhila ama aumiaye daima hukumbuka.

Dhima: Kuonya wale watu wanaosahau wema wanaotendewa.

**57. Methali:** ***Suwenyu, nsuwenyu nakabha kaghundo nsuwenyu Kemwe***

Tar- jama: Baba ni baba hata kama ni mtu mdogo au wa hali ya chini namna gani ni baba tu.

Maana: Anayeteuliwa na mwenye mamlaka apaswa kuheshimiwa hata kama anaonekana hastahili.

Dhima: kuheshimu mamlaka yaliyopo hata kama kiongozi ni mdogo kiasi gani kwani ndiye aliye na mamlaka juu yako.

**58. Methali:** ***Omona alagya nyuma, monkomo ya nyakuwabho.***

Tar- jama: Mwana hufuata kisogo cha mamaye.

Maana: Mtoto hufuata matendo ya mama au mlezi wake, hivyo akiwa mbaya au mzuri hayo ndiyo aliyoyapata toka kwa mlezi wake

Dhima: Kutahadharisha walezi/ wazazi kuwapa malezi bora.

**59. Methali:** ***Ling'ana ŕetaho/rebhore retakwatya bwatohë***

Tar jama: Neno kama halipo haliwezi kuvunja mtumbwi.

Maana: Matamshi yanapotolewa, yawe mema au mabaya hayafai kubadilishwa kwani yamekwishasikika, hivyo ni vema tuwe waangalifu katika mambo yanayozungumzwa.

Dhima: Kilichokwisha semwa kiheshimiwe maamuzi

yakishatolewa hakuna budi yatekelezwe/ yaheshimiwe.

**60. Methali:** ***Keno kikusha kubusyo bwaho tikubhune beghorihë***

Tar – jama: Kinachokuja mbele yako, hakiwezi kuvunja shingo yako.

Maana: Mara nyingi hatari inayojitokeza mbele yako, huwezi kuikwepa kwa namna yoyote ile.

Dhima: Matatizo yanayojulikana mbele yetu hatuna budi kuyakwepa.

**61. Methali:** ***Eng'ombe enkoro tekobhotorwa materahë***

Tar – jama: Ng'ombe aliyekomaa hakatwi pembe.

Maana: Unapomfunza mtoto adabu mfunze akiwa bado mdogo akikomaa hawezi kufundishika tena.

Dhima: Hutumika katika malezi/ wazazi kuwafunza maadili watoto wakiwa bado wachanga sio kusubir iw akishakomaa.

**62. Methali:** ***Enkoroiyhomwona, tekohonshokeraahe***

Tar- jama: Roho ni kama mtoto huhitaji kurudiwa jambo

Maana: Kama mtoto alelewavyo na kukoselewa mara kwa mara twapaswa kuzikanya roho zetu dhidi ya uovu.

Dhima: Kila mmoja wetu hajakamilika, hivyo ni vema kukubali kurekebishwa.

**63. Methali:** ***Inswe! Ughiringe ekerenge mbese***

Tar – jama: Samaki mkunje angali mbichi

Maana: Mtoto afunzwe adabu akiwa bado mdogo, akikomaa hatafundishika.

Dhima: Hutumika katika malezi.

**64. Methali:** ***Inswe hana yaghunda, ghonswe nkughundagere***

Tar- jama: Samaki mmoja akioza huoza wote

Maana: Kosa atendalo mtu huweza kuathiri ama kuchafua sifa hata za ambao hawakuhusika nalo.

Dhima: Hutumika kwa kuonya watu wazima na watoto wanapofanya urafiki nawenzao wabaya.

**65. Methali:** ***Urusiko uruya nyiko Ikomahekana***

Tar – jama Siku nzuri njema huonekana asubuhi.

Maana: Jambo jema huonekana mapema hata kwa namna linavyoanza, au mtu anapoambiwa kuwa ni mwema huonakana tangu utotoni

Dhima: Hutumiwa na watu wanapogundua ubaya wa jambo kuonyesha kuwa halitafaulu.

**66. Methali:** ***Urusiko urukukwa engobwe, emete ghosigho nkotera Ghere***

Tar – jama: Siku ya kufanyani miti yote hutereza.

Maana: Siku ya balaa kila msaada unaotafutwa huupati.

Dhima: Kuwatahadharisha wale wote wanaojiamini kuwa hata siku mojahawawezi kupata balaa hivyo ni vizuri kujihadhari na lolote linaloweza kujitokeza.

**67. Methali:** ***Orobhere rwe ing’ere torokokamwa buyahë***

Tar – jama: Titi la nyati halikamuliwi kwa kubembelezwa (staha).

Maana: Unapopambana na mtu mwovu au mtu wa hatari yakupasa usimwonee haya, wala kuogopa hadhi yake yapaswa kumdhibiti vilivyo la sivyo ataakurudia na kukudhuru.

**68. Methali:** ***Hano watuna kwita righoghe otakaremaha kubhusyohë***

Tar – jama Ukitaka kumua nyani, usimwangalie usoni.

Maana: Ukitaka kurekebisha jambo/ kukemea uovu, usibembeleze toa maamuzi mara moja na kuonesha msimamo wako.

Dhima: Hutumiwa hasa kwa viongozi kukemea/kuonya wale wanaowaongoza ilikuondokana na tabia iliyojitokeza na ili waongozwa wajue msimamo wako. Pia methali hii inaweza kutumika kwa mzazi/ walezi katika kukemea jambo baya.

**69. Methali:** ***Ikisire kena ketana omukwane tekekogheshahe***

Tar – jama Shoka lisilokuwa na mpini halichanji kuni

Maana: Huwezi kufanya lolote kama huna nyenzo timilifu ili kufanikisha jambo au shughuli, hivyo ili mtu aweze kutimiza jambo ni lazima ahitaji uwezo au mbinu maalumu.

Dhima: Kuthamini akiba tulizo nazo/ chochote ulicho tunza ni akiba hivyo vema kukilinda.

**70. Methali:** ***Inkuru hano Ihinya ne ng'ana enayo***

Tar – jama Kobe akiinama, ana jambo lake

Maana: Umwonapo mtu amekaa kimya usidhani kashindwa, huenda anapanga kukuangamiza.

Dhima: Kujihadhari na watu wanaokaa kimya bila kusema kitu.

**71. Methali:** ***Otakahuta Omoro han'gi neeketara kyu ubunyaki***

Tar – jama: Usipulize moto karibu na ghala lililojengwa kwa nyasi.

Maana: Usijaribu kumsemesha mtu yeyote aliye na hasira, kwani hasira zinaweza kumalizikia kwako.

Dhima: Kujihadhari na watu walio na shari.

**72. Methali:** ***Gheghaini hano ghitana nu ubunyanki bhukunyahareka***

Tar – jama: Wapiganapo fahari wawili ziumiazo ni nyasi

Maana: Ugomvi hauna malumbano kati ya watu wenye hadhi zilizosawa huleta madhara hata kwa wasiohusika.

Dhima: Kujihadhari na migogoro/mivutano katika jamii tunakotoka.

**73. Methali:** ***Righe terekubhumara ng'oko hë***

Tar – jama: Yai haliatamii kuku.

Maana: Aliye mdogo anapaswa kumsikiliza na kufuata maelekezo ya mkubwa na si kujifanya yeye ndiye anayejua.

Dhima: Kuheshimu wenye mamlaka/wakubwa.

Jumla ya methali 54 zimewasilishwa katika sehemu hii kuthibitisha kwamba dhima ya methali katika kuelimisha jamii ni pana mno. Masuala ya kuelimisha jamii kupitia methali hizi ni mengi lakini sisi tueleze kidogo kuhusu umuhimu wa kuheshimu mamlaka zilizopo kwa lengo la kuimarisha mahusiano mazuri katika jamii (Sengo, 2012). Hili linaelezwa katika methali namba 74 kwamba ni muhimu kwa kila mtu katika jamii kuhakikisha kwamba anatii mamlaka zilizopo ili mwisho wa siku maisha yawe mazuri kwa kila mtu.

Methali hii ina uhalisia katika maisha ya leo kwani watu wengi hawatii mamlaka zilizopo na kusababisha matatizo katika jamii. Kwa mfano, watu wengi wakiwemo wafanyabiashara wakubwa wanakwepa kulipa kodi na kuisababishia serikali hasara. Si kwamba serikali inapata hasara halafu basi, bali inakosa fedha za kugharimia

miradi ya maendeleo kama vile kutoa elimu, huduma za afya, maji, umeme, miundo mbinu na nyinginezo. Hali hii huchangia kuwa na umasikini katia jamii.

Kwa mujibu wa maelekezo ya nadharia ya Sosholojia ni kuwa mamlaka katika jamii huwekwa ili kuhakikisha kwamba watu wanaishi kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu ili kudumisha amani katika jamii (Scott, 1995). Inapotokea watu hawatii mamlaka ambazo zipo ni wazi kwamba amani itatoweka katika jamii. Hivyo, ni jambo la busara kila mtu kuhakikisha anatii mamlaka zilizopo kwa faida yake na ya jamii pia. Mathalani katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelezwa kuwa watu wote ni sawa na wanayo nafasi sawa katika kutoa maoni na mawazo ambayo yanapaswa kuheshimiwa.

Methali namba 27 inathibitisha hili kwamba, masikini hata akiwa na mawazo mazuri hakuna mtu ambaye atasikiliza mawazo yake na badala yake yale ya tajiri hata kama si mazuri ndiyo yatakayochukuliwa. Jambo hili si jema kwani linaondoa ile dhana ya kwamba watu wote wanayo fursa sawa katika kutoa maoni. Na badala yake kuwa kwamba ni matajiri tu ndio wenye nafasi hiyo. Mambo haya yanatokea katika jamii ya leo na kuwakatisha tamaa watu maskini kutoa mawazo na maoni yao juu ya mambo mbalimbali yanayowahusu na kuwaacha matajiri wawaamulie.

Dhima nyingine ya methali za jamii ya Wasimbiti ni kuhimiza wanajamii kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kuepuka utegemezi. Dhima hii inawasilishwa kama ifuatavyo:

### 4.2.3 Kufanya kazi kwa Juhudi na Maarifa

Methali nyingi za Kisimbiti zinasisitiza umuhimu wa wanajamii kujituma katika kufanya kazi na kuacha uzembe na utegemezi unaosababisha jamii nyingi kuwa za watu maskini ambao ni ombaomba. Serikali zote zilizowahi kutawala Tanzania zimekuwa zikihimiza wananchi kufanya kazi kama msingi wa kujiletea maendeleo. Kitogo (2002) alipokuwa akichambua siasa katika mashairi ya Saadan Kandoro anaeleza kwamba, mshairi huyo wa mashairi ya Kiswahili ametunga mashairi mengi ya kuhimiza wananchi kufanya kazi kama njia ya kuunga mkono sera ya Azimio la Arusha iliyowataka wananchi kukaa pamoja na kufanya kazi (Nyerere, 1967). Serikali ya awamu ya tano nayo pia imekuwa ikisisitiza wananchi kufanya kazi ambapo hivi karibuni imekuja na kauli mbiu ya "Hapa Kazi Tu." Kauli mbiu hii imeanza kutafsiriwa kwa vitendo ambapo hivi sasa kazi zinafanyika katika sekta mbalimbali. Methali za Wasimbiti nazo haziko nyuma katika kuhimiza watu kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kama zinavyojibainisha hapa chini:

**74. Methali:** ***Nyataita nkotokerare anyore***

Tar – jama: Mtembea bure si sawa na mkaa bure.

Maana: Anayejitahidi kujishughulisha hakosi hata siku moja kupata riziki yake kutokana na mahangaiko yake kuliko mkaa bure, hajishughulishi na chochote anasubiri kuletewa tu.

Dhima: Jamii ione umuhimu wa kujishughulisha ili kupata riziki kuliko kukaa tu au kuwa na tabia ya ukupe (tegemezi)

**75. Methali:** ***Ekitubha ketakwanga nyenyihe***

Tar – jama: Kibakuli cha kitoweo hakikatai aina yoyote ya mboga/kitoweo.

Maana: Unapokuwa na wadhifa/au mkubwa yeyote au kuwa na mamlaka,uwe tayari kuvumilia usumbufu utakaosababishwa na waliochini yako.kwani katika mamlaka hayo, utapokea mema na mabaya, na utawaongoza wema na wabaya, wapo watakaokupenda na kukuchukia.

Dhima: Kuwajasiri katika kuongoza jamii unayoitawala.

**76. Methali:** ***Onoyana embeho numwene akwikomorera***

Tar – jama: Mwenye baridi husogea penye moto.

Maana: Mtu anayehitaji jambo hana budi kuligharamia hadi kupata anachohitaji, au mwenye uhitaji hujitahidi kutafuta ufumbuzi wa shida yake wala hasubiri kuelezwa anachopaswa kufanya, husaka mwenyewe.

Dhima: Kuwa na bidii ya kutafuta mwenyewe sio kutafutiwa. Methali hii inahimiza kujitegemea na kuacha uvivu.

**77. Methali:** ***Omonto nkolyare koleng'ana nenda yaye***

Tar – jama: Mtu hula kulingana na uwezo wa tumbo lake

Maana: Mtu yeyote hufanya jambo lolote kulingana na uwezo wake,nguvu yake aliyonayo, kifedha, nguvu na mengineyo.

Dhima: Kuhimiza jamii kutafuta, mali kwa maarifa mazuri, kulingana na uwezo ulionao.

**78. Methali:** ***Singa nekebhago kyane kera nenakyo, singa kyabatongie***

Tar – jama: Ningekuwa na jembe langu lile dogo ningewazidi/ ningezidisha juhudi ya Kulima.

Maana: Mtu akishindwa kufanya jambo hutoa visingizo, hata kulaumu wenginekwakushindwa kwake.

Dhima: Hutumiwa kwa watu/mtu anayelalamika kuwa hana vifaa vya kufanyia kazi fulani ingawa ana kifaa kizuri sana cha kufanyia kazi.

**79. Methali:** ***Ekebhago ketakubhuta molemohe***

Tar – jama: Jembe halimtupi mkulima

Maana: Anayekuwa na bidii ya kazi daima hakosi kupata ujira wake/anayejibidisha au kujishughulisha na kutafuta hakosi kupata kinachamfaa

Dhima: Kuwa na bidii ya kazi katika maisha.

**80. Methali:** ***Inshara mboroye, umweghoto nkosona***

Tar- jama: Njaa ni ugonjwa, shibe ni mwana malevya.

Maana: Tatizo linapozuka wakati kuna tatizo jingine watu husahau kwa muda lile tatizo la mwanzo

Dhima: Kuwa tayari kuhangaika na kuumia, kwani matunda ya juhudi zakoyatakuja siku moja.

**81. Methali:** ***Ing'iti nsingunu syaye ekorya***

Tar- jama: Fisi hula kwa nguvu yake.

Maana: Kila mtu hujikomboa kwa juhudi ama uwezo alionao.

Dhima: Kuhimiza kujitegemea katika maisha siyo kuwategemezi kwa watu wengine.

**82. Methali:** ***Embori nkoreserye koreng'ana no orotambe lu urusiri rwaye***

Tar – jama: Mbuzi hula kulingana na urefu wa kamba yake.

Maana: Anyejibidisha na kutafuta riziki ya kila siku hufanikiwa kulingana namizunguko aliyozunguka au mtu hupata riziki kulingana na mazingira yake yakazi aliyonayo.

Dhima: Kuwa na bidii ya kutafuta riziki.

**83. Methali:** ***Enonkwe etakusha kobhelehë***

Tar – jama: Bahati haiji mara mbili

Maana: Unapopata fursa ama nafasi ya kutenda jambo yakupasa uitumie vema nafasi na si kuipuuzia au

kutaka usaidiwe kuipokea.

Dhima: Kuhizima watu wanaokaa tu bila kujishughulisha wakisubiri kupata neema huku wakiwa wamekaa kwani bahati haina utaratibu maalumu wakutokea, hivyo kila mmoja wetu anapaswa ajishughulishe na si kungojea bahati.

**84. Methali *Amaikaye teghakolebwahë***

Tar – jama: Kitako hakiliwi

Maana: Kuwa na mtu mwenye shida na kukaa naye tu bila kumpa ufumbuzi huwezikumsaidia,hivyo hakuna budi kumpa ufumbuzi wa kutaka kujituma na kufanya kazi, kwani kukaa kitako bila kufanya kazi au kutafuta ufumbuzi mwingine wa kupata riziki ni kuleta balaa katika nyumba.

Dhima: Bidii katika kazi.

**85. Methali: *Lelo ndelo omoghambi wa Isho no molongo***

Tar – jama: Leo ni leo msema kesho ni mwongo.

Maana: Ikiwa jambo linaweza kufanyika sasa ni vyema likafanyika kwani hakuna uhakika wa hali ilivyo hapo baadaye.

**86. Methali: *Eng'ombe iya mbele yho ikunywa amanshe amalabhu***

Tar- jama: Ng'ombe ya mbele ndiyo inywayo maji safi.

Maana: Anayetumia fursa pindi tu ipatikanapo ana nafasi nzuri zaidi yakufanikiwa, vile vile ubora wajambo hutegemea uzuri wa hatua yake ya mwanzo. Au kutangulia kufanya jambo kuna faida nyingi, kwani unapozembea ama kuchelewa kutenda jambo huishia kumfanya mtu kukosa vilivyo vizuri.

Dhima: Kuhimiza jamii kuacha uzembe, na kutumia fursa tunazopata kwa muda unaotakiwa sio kungonja kesho au siku nyingine.

**87. Methali:** ***Omoremi takukura nsharahë***

Tar- jama: Mkulima hodari halii njaa

Maana: Anayejishughulisha kwa bidii katika kazi hakosi kupata riziki kila siku si sawa na yule anayekaa tu na kusubiri kuletewa na kuomba omba.

Dhima: Kuwa na bidii katika kazi siku zote.

**88. 89. Methali:** ***Ono akorema ko mobhaso, Mkiriri akunyera***

Tar – jama: Mlimia juani hulia kivulini

Maana: Mara nyingi watu hawapendi kujishughulisha ili kufanikisha jambo lakini yule anayevumilia taabu zakupata kitu fulani, hufurahia baada ya kupata mafanikio yake. Hivyo anayekubali kujishughulisha

mwishowe atapata riziki na ahueni katika maisha yake.

Dhima: Kuwakumbusha wanajamii kuwa na bidii ya kazi kwa sababu mtu kupata riziki au mafanikio ni matokeo ya juhudi yake katika kazi.

**89. Methali:** ***Hano omote ghotaho, ikiriri tekehohë***

Tar – jama: Bila kuwepo na mti, kivuli hakiwezi kuwepo.

Maana: Tusibweteke na manufaa tupatayo kutoka katika vitu mbalimbali tukasahau kuwa manufaa hayo hutokana na uwepo wa vitu vinavyoleta ama juhudi za watu.

Dhima: Kusisitiza jamii kuwa na bidii katika kazi kwani jambo unaloanza leo hata kama ni dogo/dhaifu linaweza kuwa kubwa zaidi hapo baadaye

**90. Methali:** ***Umutunyo gho omoswa ghorahaghasha inyumba yabho na amate ghabho***

Tar- jama: Bidii ya mchwa hujenga nyumba kwa mate.

Maana: Juhudi humwezesha mtu kufanikisha hata mambo yaliyo makubwa yaonekanayo magumu.

Dhima: Bidii katika maisha.

**91. Methali:** ***Ikyabhosa nkya Ighori***

Tar- jama: Chabure ni gharama

Maana: Usipende vya kupewa bila kugharamia kwani waweza kudaiwa ama kudhalilishwa kwa sababu ya kupewa msaada.

Dhima: Weka juhudi katika maisha.

**92. Methali:** ***Obhosa bhorarosya***

Tar – jama: Bure huchosha.

Maana: Tusijizoeshe kupenda kupokea vitu bila kuvitokea jasho tukiwa hivyo tutawakwaza wanaotupa, ama wao wakatusema vibaya na kutukera.

Dhima: Kujitegemea mwenyewe/ kujitahidi kujitafutia mali yako mwenyewe bila kutafutiwa na wengine

**93. Methali:** ***Ikyo kobosha tikyakwibhahë***

Tar- jama: Chakuokota si cha kuiba

Maana: kisichokuwa na mwenyewe waweza kukimiliki kwani kingekuwa cha mtu lazima angekilinda au kukitetea.

Dhima: Tafuta vyakwako si kutegemea kuokota tu.

**94. Methali:** ***Ikyokohanwa tikyanehë***

Tar – jama: Chakupewa si chako

Mana: Usitambe au kubweteka na mali isyokuwa yako, weka juhudi utafute vyakwako, kwani kinaweza kuchukluliwa wakati wowote.

Dhima: Kujitahidi wakati wowote kujitafutia mali yetu wenyewe bila kutegemea sana vya wenzetu.

**95. Methali:** ***Ikya abhene na bhene byakokerya.***

Tar- jama: Cha wenyewe huliwa na wenyewe.

Maana: Aliyekifanyia kazi kitu na kukipata ndiye mwenye haki na mamlaka ya kukitumia katika maisha yake na sivinginevyo.

Dhima: Usitegemee kula usivyotafuta wewe jitegemee.

**96. Methali:** ***Okobhoko kurenge bhosa teghokorebwahë***

Tar – jama Mkono mtupu haulambwi.

Maana: Asiyeweza kuwafaa. Wengine hawezi kutegemewa kwa msaada wala kupewa heshima.

Dhima: Jitihada binafsi zinaweza kufanikisha jambo Fulani.

**97. Methali:** ***Makayeiwa teghakorebwahe***

Tar – jama: Uvivu hauliwi.

Maana: Matokeo ya uvivu ni umaskini kwani humkosesha mtu nafasi ya kujipatia vilivyo vyema ama vizuri.

Dhima: Kutoendekeza uvivu.

**98. Methali:** ***Ikisire ikyo uwonde tekekomara moremohe***

Tar- jama: Shoka lisilo lako haliwezi kumaliza kazi yako.

Maana: Huwezi kutegemea vya wengine ili kutimiza haja zako kila mara. Weka juhudi ili kujipatia mahitaji yako.

Dhima: Kuwa na tabia ya kuwa na vyako. jiwekee akiba yako sio kutegmea vya wengine au jirani yako.

**99. Methali:** ***Ubhumura no omoki tubhu kukyorahë***

Tar- jama: Ujana si jambo la kudumu, hufika muda ujana huisha.

Maana Ujana ni moshi, uendapo haurudi tena

Dhima: Kuwakumbusha vijana kutumia muda vizuri na ujana haudumu milele, huja ukafikia mwisho.

**100. Methali:** ***Hano ubinyore oberya, hano utabinyore ubhihita.***

Tar – jama Ukipata kitumie, ukikosa kijutie

Maana: Unapopata kitu ama fursa ya kufanya jambo tumia kwa ufanisi kwani yawezekanafursa hiyo isiwepo milele.

Dhima: Tumia vizuri muda ulio nao kutenda mema.

**101.Methali** ***Kyakwasagharibwa, tekekomarabhotobhuhe***

Tar – jama: Kitu cha kuazima hakimalizi shida yako

Maana: Huwezi kujivuna na kitu cha kuazima kwani si chako na mwenyewe anaweza kuja kukichukua wakati wowote.

Dhima: Kutahadharisha watu ili kuwa na tabia ya kujitafutia mali zao mwenyewe bila kutegemea sana vya watu.

**102. Methali:** ***Umughi gho Omorosu toghona ketarehë***

Tar – jama Mji wa mtu aliye mvivu, hauna ghala.

Maana: Uvivu na uzembe husababisha umaskini, kwani mtu hushindwa kufanya mambo ambayo pengine yangempa riziki.

Dhima: kutofanya uzembe na mizaha kwani huleta umaskini katikafamilia.

Katika sehemu hii inayozungumzia dhima ya kufanya kazi kwa juhudi na maarifa jumla ya methali 28 zimewasilishwa. Methali hizo kwa ujumla wake zinahimiza kuwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ni jambo la muhimu katika kuhakikisha kuwa jamii inapata maendeleo. Methali namba 75 inaeleza kuwa si jambo la busara kwa watu kukaa na kujibweteka bila ya kufanya kazi kwa kisingizio cha kukosa kazi ya kufanya.

Si kweli kwamba katika jamii hakuna kazi za kufanya bali watu ndio wanaochagua kazi za kufanya. Methali inasema, “mtembea bure si sawa na mkaa bure,” ikiwa na maana kuwa ikiwa mtu atatoka nyumbani kwake asubuhi kwa lengo la kutafuta kazi

ya kufanya ataipata kazi hiyo na kupata ujira ambao utasaidia wale wanaomtegemea. Methali namba 80 inashadadia kuwa kila mwenye kufanya jitihada katika kufanya kazi mara nyingi hufanikiwa kuwa na maisha mazuri.

Nadharia ya Sosholojia inasisitiza kwamba ni wajibu wa kila mwanajamii kufanya kazi yake kwa jitihada ili kuleta tija kwake binafsi na taifa kwa jumla (Webster, 2006). Imezoeleka kuona watu wakipenda kulipwa mishahara na marupurupu makubwa lakini kazi hawafanyi. Hii huchangia katika kufanya jamii iendelele kuwa maskini na hivyo tabia kama hii inatakiwa kuachwa mara moja.

### 4.2.4 Kuhimiza Umoja na Mshikamano

Kuhimiza Umoja na mshikamano ni moja kati ya dhima muhimu ya kazi za fasihi simulizi tangu karne na karne mpaka hivi sasa. Tunapotazama kazi kama hadithi katika fasihi simuli tunaona zikizungumzia umuhimu wa kuwa na umoja na mshikamano katika kufanya kazi na kusaidiana katika kutatua changamoto mbalimbali za maisha (Sengo, 2009).

Viongozi wa kisiasa nao wamekuwa wakihimiza juu ya umoja na mshikamano kuwa ndio njia pekee ya kupambana na maadui watatu ambao ni njaa, maradhi na ujinga. Utanzu wa methali nao umeliona suala la umoja na mshikamano kuwa ni la muhimu sana ndio maana hata Waswahili husema kuwa “umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.” Methali za Kisimbiti zinazozungumzia umuhimu wa umoja na mshikamano ni nyingi kama zilivyoowasilishwa hapa chini:

Ushirikiano/mshikamano na umoja husisitiza kufanya mambo kwa pamoja ili kuleta maendeleo katika jamii ya Wasimbiti. Methali zifuatazo zinasisitiza umoja na ushirikiano; methali hizo ni,

**103. Methali:** ***Ono ataho ni lyaye telehohë***

Tar – jama: Asiyekuwepo na lake halipo

Maana: Mtu asiyekuwepo mahali husahauliwa na huenda asikumbukwe kwayale yanayoendelea.

Dhima: Tunakumbushwa kwamba tukitaka kufanyiwa jambo fulani sharti tuwepoau kushiriki katika utendaji la sivyo maslahi yetu hayatazingatiwa.

**104. Methali:** ***Osore mbonswe, tomanyire ono alekobhekahë***

Tar – jama: Jali watu wote usipendelee wako tu.

Maana: Usipuuze watu usiowafahamu na kuwadharau kwani upo umuhimu wao kwako, kwani kuna wakati utawategemea, kwani kumbuka umaarufu wako wa leo, kesho hupotea.

**105. Methali:** ***Omong'aini (takwikebhahë) tikebhe mwenehë***

Tar – jama: Mwerevu hajinyoi.

Maana: Hata ukiwa na uwezo na akili kiasi gani huwezi kujitimizia haja zako zote, wanadamu hutegemeana.

Dhima: Kukumbusha jamii kuwa binadamu hutegemeana, hakuna mtu anayejitosheleza peke yake

**106. Methali:** ***Mokari wanda takwimwa kentohë***

Tar – jama: Mjamzito hanyimwi kitu.

Maana: Kuwathamini wote waliona na shida leo, na kuwasaidia kwa hali na malikwani mjamzito ni muhitaji muhimu asiyepaswa kunyimwa huduma haraka.

Dhima: Kuwathani wenye mahitaji ya lazima.

**107. Methali:** ***Ono atamanyire obasani temosani wo bhandehe***

Tar – jama: Asiyefahamu urafiki si rafiki

Maana: Asiyejua gharama ama wajibu wa rafiki basi hawezi kuwa rafiki bora.

Dhima: Kuhimiza upendo/kuthamini urafiki na upendo katika jamii.

**108. Methali:** ***Ikiya tekekokorahë***

Tar – jama Chema hakidumu.

Maana: Mtu mema mara nyingi hadumu na aliye katiri ndiye hudumu.

Dhima: Hutumiwa kwa watu wanaomlilia yule waliyempenda kwa mazuri aliyowafanyia katika uzima wake.

**109. Methali:** ***Ikyaro na abhanto***

Tar – jama: Dunia ni watu

Maana: Kushirikiana na watu/jamii ni vizuri kwani ndio wenye uwezo wakukufanikishia au kukuharibia mambo yako.

Dhima: Kuonya watu wasiopenda ushirikiano katika jamii, kwani hakunaanayeweza kuishi peke yake bila kuwa na msaada wa wengine.

**110. Methali:** ***Ikyara ekemwe tekekwatya enda hë***

Tar – jama Kidole kimoja hakivunji chawa.

Maana: Ili kutimiza jambo au kufanikiwa twahitaji kushirikiana na wengine.

Dhima: Kuhimiza kuwa na umoja.

**111. Methali:** ***Lighiha Limwe terekurughahe***

Tar – jama: Figa moja halipiki.

Maana: Hakuna anayeweza kuishi peke yake katika jamii akafanikiwa bila kuwepo wa pili.

**112. Methali:** ***Umuhiri waho nono akokotorya***

Tar – jama: nduguyo ni yule anayekusaidia katika shida.

Maana: Undugu wa kweli ni kusaidiana katika matatizo

Dhima: Kusaidiana katika shida na raha.

**113. Methali:** ***Ukwikara no Muhiri waho nkoremerya***

Tar- jama: Kuishi na nduguyo uwe mvumilivu lawama kujitokeza.

Dhima: Uvumilivu katika kuishi na nduguyo.

**114. Methali:** ***Umushasha ni kihita, Omokari ni imiri***

Tar- jama: Mmme ni tawi na mke ni mzizi

Maana: Mme na mke wote ni wa muhimu katika familia, mme huijenga familia na mke huleta mshikamano na upendo.

Dhima: Kuhimiza ushirikiano katika kujenga familia.

**115. Methali:** ***Amaghaini abhere teghakwikarehe igho imwe - hë***

Tar- jama: Fahari wawili hawakai zizi moja.

Maana: Watu wenye vipawa vya kufanana hawawezi kushirikiana, kwani kila mmoja atajaribu kuonesha uwezo wake kumpita mwenzake.

Dhima: Hutumiwa kwa watu wawili ambao wanashindana na wana nguvu sawa.

**116. Methali:** ***Hano waghegwa wange kwikunya***

Tar – jama: Ukibebwa usijikunjekunje

Maana: Unaposaidiwa usilemae na kujifanya tegemezi kupindukia, bali nawe onesha juhudi kujiondoa kwenye uhitaji.

Dhima: Kuonesha ushirikiano pale unaposaidiwa, lasivyo utamkatisha tamaa yule anayekusaidia.

Dhima ya methali za Kisimbiti katika kuhimiza wanajamii kuwa na umoja na mshikamano kama zilivyowasilishwa hapo juu ni 13. Methali namba 106 inaeleza kwama mtu "mwerevu hawezi kujinyoa," ikiwa na maana kuwa ipo haja ya wanajamii kushirikiana katika mambo mbalimbali yahusuyo maisha yao ya kila siku. Si jambo la busara kuona mtu akijidai ni hodari wa kufanya mambo yeye mwenyewe bila kushirikiana na wenzake. Ni ukweli ulio wazi kwamba hakuna mtu ambaye anaweza kufanya kila jambo yeye binafsi bali kwa kushirikiana na wenzake ndio mambo hufanikiwa. Wanasosholojia wanasisitiza kuwa ili jamii yoyote ile iweze kupata maendeleo ni lazima watu wafanye mambo yao kwa kushirikiana (Cross, 2011). Pale watu wanaposhirikiana ndipo ambapo mambo hufanyika vizuri kwa sababu kuna kuwa na nguvu zaidi na maarifa zaidi yanayowezesha mambo kufanikiwa. Methali hii inafanana na ile ya Waswahili isemayo, "umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu (Kunnemah, 2008). Methali namba 111 nayo inashadadia hoja ya umuhimu wa umoja na mshikamano katika jamii.

### 4.2.5 Umuhimu wa Malezi Bora katika Jamii

Kuifanya jamii kuwa na malezi bora ni moja kati ya dhima ya kazi zote za fasihi ya Kiswahili. Hii ni sawa na kusema kuwa kazi za fasihi zina dhima ya kutoa maelekezo juu ya namna bora ya wazazi kuwalea watoto wao. Katika ulimwengu wa fasihi simulizi iliaminika kwamba watoto ni mali ya jamii na mtu yeyote ambaye amefikia umri wa utu uzima ana wajibu wa kumlea mtoto yeyote yule hata kama si yeye

aliyemzaa (Mulokozi na Kitogo, 2007; Maitaria, 2010), katika kipindi hicho mtoto aliweza kudhibiwa na mtu mzima yeyote pale alipokosea. Hata hivyo katika miaka ya hivi karibuni mambo yamebadilika ambapo hivi sasa mtu mzima yeyote hawezi kumwadhibu au hata kumuonya mtoto aliyekosea ila tu kama ni mtoto wake wa kumzaa. Methali za jamii ya Kisimbiti zinathibitisha kuwa, malezi ya mtoto ni jukumu la jamii na si la mzazi peke yake. Kupuuzia jambo hili ndio maana hivi sasa baadhi ya jamii hasa watoto na vijana wengi hawana Maadili mazuri. Methali hizo zimewasilishwa, kuchambuliwa na kujadiliwa hapa chini kama ifuatavyo:

**117. Methali:** ***Nyawigholo narekoleta, nokakenya iyake!***

Tar – jama: Hata ukikimbia vipi, giza litakurudisha tu.

Maana: Hata ukikimbia matatizo vipi, kokote utakapokwenda utayakuta tu.

Dhima: Kuhimiza jamii kutokimbia matatizo, ni vyema kubaki pale pale na kuyakabiri matatizo hayo.

**118. Methali:** ***Hano otighulei lyo omokoo ekyalo kilekogoghera***

Tar – jama: Usiposikia la mkubwa, dunia itakufunza.

Maana: Anayekataa kuonywa ama anayekataa mafundisho apewayo nawakubwa/wakuu wake huishia kufikwa na mabaya ambayo kama angesikiliza pengine angeyaepuka.

Dhima: Inawaasa watu au mtu ambaye hasikii mawaidha anayopewa na mkuu/wakuu wake, hivyo ni vema

kusikia kile unachoambiwa na wakuu wako na kuacha mabaya.

**119. Methali:** ***Okotongela abholelo neghene okotemo kolyende.***

Tar – jama: Vijana wa leo hawashauriki.

Maana: Kizazi cha leo hakishauriwa na hata Kuelekezwa chochote.

Dhima: Watoto/vijana wazingatie na kusikia yale wanayoshauriwa na wazazi/ walezi wao.

**120. Methali:** ***Umwitëë uwa orosenke, numwene akorotoora***

Tar – jama: Anayejitwika mtungi kichwani ni yeye peke yake atakayetua mtungi huo.

Maana: Atafutaye matatizo hana budi kuyatatua mwenyewe. Anayetafuta/sababisha matatizo hupaswa kuwajibika kwa madhara ya matendo yake, na unapoanzisha jambo fulani basi yakupasa kulikamilisha.

Dhima: Kujihadhari na kutosababisha matatizo katika jamii. Ni vyema kuishi vizuri kuliko kuishi na kuleta fujo, matatizo katika maisha.

**121. Methali:** ***Onoatamanyirë eng'ana tatebwibwi ng'ana hë***

Tar – jama: Asiyejua maana haambiwi maana.

Maana: Hakuna haja ya kumuelimisha mtu kuhusu thamani ya jambo analolipuuza au kutokulithamini.

Dhima: Kuthamini yale tunayoelekezwa au kuambiwa na wanaotoa elimu hiyo.

**122. Methali:** ***Onoatakwigwa agho omokoro naleboneke Okoghoro***

Tar – jama: Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.

Maana: Anayekataa makanyo ama mafundisho apewayo na wakubwa wake huishia kufikwa na mabaya ambayo kama angesikiliza pengine angeyaepuka.

Dhima: Hutumiwa kwa mtu ambaye hasikii mawaidha anayopewa na wakubwa wake.

**123. Methali:** ***Yeka iya abhaheghe niyabhaheghi***

Tar – jama: Ukoo wa wawindaji ni wawawindaji tu.

Maana: Mtu hawezi kuficha ama kubadili tabia yake kwa urahisi ni sawa na kuvua na kubadili rangi ya ngozi, au mtu, hawezi kuficha ama kuibadilitabia au mazoea yake ya lazima yatajionesha tu.

Dhima: Kujihadhari na wanafiki hata kama ni rafiki, au ndugu yako wa karibu.

**124. Methali:** ***Ikyaro tekena Ikibhisirehe***

Tar – jama: Dunia haina siri.

Maana: Si rahisi kufanya jambo lisifahamike ipo siku watu watalifahamu tu,

Dhima: kujihadhari na kuwa makini kumweleza kila mtu yeyote mambo yako ya siri kwani unaowaambia husema kwa watu wengine na mwisho ikawa sio siri tena.

**125. Methali:** ***Hano otare nu umebwi whonse nu mwebhi ore.***

Tar – jama: Ukitembea na mwizi nawe ni mwizi

Maana: Ukijihusisha na yeyote aliye na tabia mbaya, nawe utaiga tabia hizo nawe utatenda maovu yanayotendwa na hao unaojihusisha nao.

Dhima: Hutumika katika malezi, kuonya watoto/vijana kuondokana na makundiyenye tabia mbaya.

**126. Methali:** ***Iliso iryo kukwa nkukurarere***

Tar – jama: Jicho la kufa huanza kulia mapema.

Maana: Mtu au kitu kinachoelekea kuharibika huanza kuonyesha dalili mapema.

Dhima: Hutumika kwa mtu anayeanza kuonesha dalili zisizo katika tabia njema.

**127. Methali:** ***kereng'ombe ilimena no oreme ryaye mwinyero ryaye***

Tar – jama: Kila ng'ombe hutia ulimi puani mwake

Maana: Mtu mpumbavu hufanya mambo yanayoendana na tabia yake mathalana kufanya vitendo vya kujidhuru mwenyewe.

Dhima: Kuonya watu wanookwenda kinyume na maadili mema.

128. **Methali:** ***Onoatamanyirë eng'ana tatebwibwi ng'ana hë***

Tar – jama: Asiyejua maana haambiwi maana.

Maana; Hakuna haja ya kumwelimisha mtu kuhusu thamani ya jambo analolipuuza au kutokulithamini.

Dhima: Kuthamini yale tunayoelekezwa au kuambiwa na wanaotoa elimu hiyo.

129. **Methali:** ***Hano wahoya ne ekekondo nkekomara omoghondo***

Tar- jama: Ukicheka na kima utavuma mabua.

Maana: Ukiendeleza au kuvumilia uzembe mwishowe utapata hasara.

Dhima: Kemea uzembe/uovu bila kuchoka.

Katika sehemu hii inayozumgumzia dhima ya methali katika malezi tumepata jumla ya methali 12 jambo linaloashiria kwamba malezi mema katika jamii ni kitu muhimu sana. Methali namba 118 inaeleza kwamba, vijana wanatakiwa kupatiwa malezi mazuri na wazazi wao ili waweze kutatua changamoto za maisha hapo walipo badala ya kukimbilia mijini wakidhani kuwa, ndiko kwenye maisha mazuri. Imekuwa ni jambo la kawaida kuona vijana makundi kwa makundi wakitoka vijijini kwenda mijini kwa kisingizio cha kwenda kutafuta maisha. Vijana wakipatiwa malezi mazuri wanaweza kufahamu kwamba maisha mazuri hupatikana kwa mtu kufanya kazi kwa

juhudi na maarifa. Suala la kwenda mjini ndio mtu apate maisha mazuri halina ukweli kwani maisha ya mjini ni magumu kulio ya kijijini. Mtafitiwa mmoja alieleza kwamba:

> *Wazazi wa siku hizi hawako makini katika malezi ya watoto wao kama ilivyokuwa hapo zamani. Unakuta mzazi hawezi kukaa na mtoto wake akazungumza naye kuhusu maisha. Mtoto anafanya yakwake na mzazi anafanya yake ndio maana kijana akifikisha umri wa kujitegemea anashindwa na badala yake anaona maisha kuwa ni magumu sana. Suluhisho la maisha magumu analolipata kwa haraka ni kwenda mjini kwani huko ndio kwenye maisha mazuri. Baadhi ya vijana huamua kujiingiza katika unywaji wa pombe hasa pombe haramu kama njia ya kupunguza mawazo yaletwayo na maisha magumu katika jamii. Mambo yote haya yasingelitokea kama kijana angepatiwa malezi mazuri na wazazi wake na jamii inayomzunguka. Siku hizi suala la malezi ya watoto limeachwa kwa wazazi na walezi peke yao jambo ambalo si sahihi sana. Jamii nzima ni lazima iwajibike katika kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata malezi bora ili baadaye tuwe na vijana na wazee wenye Maadili mazuri katika jamii.*

Maelezo ya mtafitiwa hapo juu yanaonesha kwamba vijana wanatakiwa kupata malezi mazuri ili waweze kukabiliana na changamoto za maisha. Mawazo haya yanashadadiwa na methali namba 119 ambapo inaeleza kuwa kila mwanajamii hasa watu wazima wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata malezi mema hata kama si kwa mtoto wake wa kumzaa. Malezi kwa mtoto ni jukumu la watu wote katika jamii na si jukumu la mzazi au mtu mmoja pekee (Maitaria, 2012). Mawazo haya yana uhalisia katika maisha ya kila siku ya jamii kwani pale ambapo mtoto anapatiwa malezi mazuri huwa na misingi mizuri ya kumfanya aishi maisha mazuri wakati wa ujana na utu uzima wake. Vijana wengi ambao hawakupata malezi mazuri wakati wa utoto wao ndio wengi kati ya wale wanaokimbilia mjini kutafuta maisha mazuri. Methali namba 130 inasisitiza kwamba ni vema kila mwanajamii akakemea jambo baya litakalokuwa linafanywa na mtoto yeyote yule ili ajifunze

kwamba kufanya hivyo ni vibaya na aache. Haya ndiyo malezi mema ambayo kila mtoto anatakiwa apatiwe na wazazi pamoja na jamii inayomzunguka.

## 4.3 Mbinu za Kisanaa katika Methali za Kisimbiti

Mbinu za kisanaa ni ule ufundi wa kisanaa unaotumika katika kuijenga kazi ya fasihi na kuwa katika umbo ililonao (Njogu na Chimerah, 1999). Mbinu za kisanaa hujidhihirisha kutokana na vipengele vya kifani kama vile muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha. Vipengele hivi vya kifani ndivyo vinavyotumika si katika fasihi simulizi peke yake bali pia katika fasihi andishi. Methali ni kijitanzu katika utanzu wa semi uliopo katika fasihi simulizi. Utanzu huu una matumizi ya mbinu mbalimbali za kisanaa ambazo kwazo ndio dhima ya methali inapodhihirika kwa wasikilizaji au wasomaji wa methali husika. Tunaanza na matumizi ya mafumbo kama mbinu ya kisanaa katika kuwasilisha dhima ya methali za Wasimbiti.

### 4.3.1 Lugha ya Mafumbo katika Methali za Kisimbiti

Mafumbo ndio mbinu kubwa ya kisanaa inayojitokeza katika methali si za Wasimbiti tu bali za jamii zote duniani (Senkoro, 2006). Lugha ya mafumbo si sifa ya methali peke yake bali ni sifa ya aina zote za semi ikiwa ni pamoja na vitendawili, nahau, misemo na misimu. Tunaweza kusema kuwa mafumbo ndio uti wa mgongo wa semi. Methali karibu zote zimejengwa kwa kutumia lugha ya mafumbo ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Wakati mwingine, methali inaweza kuwa na lugha ya kawaida kabisa lakini yanayoelezwa kupitia lugha hiyo yameelezwa kwa mafumbo. Hebu tuone methali ifuatayo kutoka jamii ya Wasimbiti:

**Methali:** *Hano wegegwa, wange kwikunya*.

**Tarjama:** Ukibebwa, usijikunjekunje.

Methali hii imejengwa kwa kutumia fumbo ambalo linamtaka msomaji au msikilizaji kuwa makini kidogo ili aweze kuelewa ni jambo gani linalosemwa katika methali hii. Lugha iliyotumika katika methali hii ni ya kawaida sana lakini ndani yake mna fumbo kali. Methali hii inawalenga watu ambao husaidiwa lakini hawasaidiki kwa sababu ya kurudi nyuma. Methali hii inaonya kwamba mtu ambaye anasadiwa kwa njia moja au nyingine anatakiwa kuonesha kweli yupo tayari kusaidiwa. Kwa mfano, mtu anaweza akaamua kumchukuwa mtu kutoka kijijini akamleta mjini na kisha akampeleka shule na kulipa ada zote zinazotakiwa. Jambo la kushangaza ni kuwa yule aliyepelekwa shuleni hana habari na ndio kwanza kila siku anatoroka shule.

Waswahili wana methali yao inayofanana na hii isemayo, "abebwaye hujikaza." Mtu anaposaidiwa ni wajibu wake kuhakikisha kuwa anatekeleza yote anayoelezwa na mtu anayempatia msaada ili hatimaye aweze kufanikiwa katika msaada huo. Ikiwa mtu atabebwa mgongoni kwa mtu mwingine halafu hata hajishikilii bila shaka atampa taabu kubwa mbebaji na upo uwezekano akaangushwa chini. Methali hii imejengwa kwa kutumia lugha yenye taswira ndani yake kupitia msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki (Mark, 1995). Kuielewa vizuri methali hii mtu anatakiwa atazame tukio la mtu kubebwa mgongoni mwa mtu na kisha alifananishe tukio hilo na methali iliyopo hapo juu. Tukio la mtu kubebwa mgongoni mwa mtu mwingine ni la kawaida lakini hapa limetumika kifasihi kwa lugha ya mafumbo kuwasilisha ujumbe mzito kwa wasomaji au wasikilizaji wa methali hii.

#### 4.3.2 Matumizi ya Takriri

Khatibu (1986) anasema, Takriri ni usemi unaojidhihirisha katika neno au kifungu cha neno kwenye mfululizo na mfuatano wa sentensi. Takriri ni mojawapo ya stadi za kisanaa katika tanzu za fasihi ya kiswahili. Mtumiaji/Mtunzi hurudiarudia neno au maneno au silabi fulani ya neno akilenga kulitilia mkazo au msisitizo wa jambo fulani, hivyo hurahisisha jambo linalosemwa na kunata akilini mwa msikilizaji. Matumizi ya takriri ni moja kati ya sifa muhimu ya lugha inayotumika katika fasihi simulizi ya jamii zote duniani. Takriri hutumiwa ili kutoa msisitizo wa dhamira fulani kwa hadhira iliyokusudiwa.

**Methali:** *Wenyu wenyu* hakabha haghogho, wenyu tohangehe

**Tarjama:** Kwenu ni kwenu, hata kama ni pabaya ni kwenu.

Katika methali hii kuna matumizi ya takriri ambapo neno “wenyu” limerudiwa mara tatu kutoa msisitizo kwamba kwenu ni kwenu hata kama ni kubaya. Methali hii inatoa msisitizo kwamba ni vema watu wakathamini na kujali nyumbani kwao kwa kuwa mtu hawezi kuwa na mahali pengine anapoweza kupaita kuwa ni nyumbani kama pale mahali alipozaliwa. Imetokea katika jamii nyingi si ile ya Wasimbiti peke yake, baadhi ya watu huondoka nyumbani kwao kwa muda mrefu na kuwaacha wazazi wakiteseka bila msaada wa aina yoyote. Baada ya muda mtu wa aina hiyo anapopatwa na matatizo hulazimika kurejea nyumbani na wakati mwingine hurejeshwa akiwa tayari amefariki.

Waswahili wana methali yao inayofanana na hii inayosema kwamba, “nyumbani ni nyumbani hata kama ni juu ya mti. Baadhi ya watu husahau nyumbani kwao kwa

sababu ni pabaya na hudhani kwamba huko walipolowea wataishi milele. Jambo la msingi hapa ni kwamba kila mtu anapaswa kujali na kuthamini nyumbani kwao na afanye juhudi na maarifa ili kupaimarisha pawe pazuri.

Matumizi ya takriri yanajitokeza katika methali nyingi za jamii ya Kisimbiti kutokana na hali halisi kwamba methali hutumika katika kusisitiza mambo muhimu katika maisha ya binadamu. Methali ifuatayo ina matumizi ya takriri.

**Methali:** *Akake kake, kara* mara eketara.

**Tarjama:** Kidogo kidogo, humaliza ghala zima.

Katika methali hii neno “kake,” likiwa na maana ya kidogo katika lugha ya Kiswahili limerudiwa mara mbili na hivyo kusomeka, “kidogo kidogo.” Matumizi ya takriri hii yametumika kwa lengo la kutoa msisitizo kwamba ni vizuri kutumia mali iliyopo kwa umakini. Inafahamika kwamba kadri mali hiyo inavyotumika ndivyo inavyokwisha. Ni vema itumike kwa makini ili iweze kusaidia jamii kwa muda mrefu. Takriri hii imejengwa kwa kutumia lugha ya kiishara kutokana na msimbo wa kiishara wa nadharia ya Simiotiki kurejelea vitu vyote vyenye thamani vitumiwe vizuri (Eco, 1976). Mathalani, katika nchi ya Tanzania, kuna utajiri mkubwa wa madini ya aina mbalimbali lakini madini hayo yanachukuliwa na wageni ambao ni wawekezaji kutoka nje ya nchi kwa manufaa yao na si manufaa ya jamii ya Watanzania. Baada ya miaka michache ijayo madini hayo hayatakuwepo tena na nchi itakuwa imepata hasara kubwa. Methali hii inafanana na ile ya Kiswahili isemayo, “bandu bandu humaliza gogo.”

### 4.3.3 Matumizi ya Taswira

Taswira ni picha anayoipata msomaji mara baada ya kusikia maneno au kuona jambo fulani lililopitishwa mbele yake. Kuhenga (1977) anasema taswira ni mpangilio wa maneno katika kujenga picha za hisia katika mawazo au zinazoonekana (halisi) picha za kuhisi zinazompa msomaji /msikilizaji mguso wa kimwili kutokana na mitajo ya vitu au matukio fulani, kwa mfano: tukio la kuchomwa sindano kali; msikilizaji/ mtazamaji atahisi jinsi mtu anavyopata maumivu mwilini mwake.

**Methali:** Risarighoko, terekorera bhanahe.

**Tarjama:** Jogoo, hawezi kulea wana.

Methali hii inajenga taswira kwa mtu ambaye tayari anafahamu suala la malezi ya watoto katika jamii limeachwa kwa nani. Kimsingi, mama ndiye mwenye jukumu kubwa katika malezi ya watoto kuliko baba kwa kuwa mama ndiye anayekuwa na watoto kwa muda mwingi. Imekuwa si jambo la kawaida kuona baba akitumia muda mwingi kukaa na watoto kama ilivyo mama kiasi hata baadhi ya wanaume huamini kuwa si jukumu lao kulea watoto. Mtoto hasa anapokuwa mdogo ni msumbufu wa mambo mengi ambayo yanahitaji utulivu na uvumilivu katika kuyatimiza. Ni mama pekee ndiye mwenye uwezo huo na si baba. Tunapokutana na methali tunajaribu kuvuta taswira juu ya uzito wa kumlea mtoto na kisha tunalinganisha kati ya mama na baba nani mwenye uwezo huo. Kimsingi, ni kweli kuwa “jogoo hawezi kulea wana.”

Hata hivyo, katika maisha ya siku hizi wazazi wote, baba na mama wanahimizwa katika kusaidiana kuwalea watoto kwani mtoto anapopata malezi ya baba na mama

anakuwa na maadili zaidi kuliko yule aliyepata malezi ya upande mmoja.

### 4.3.4 Muundo katika Methali za Kisimbiti

Muundo ni moja kati ya vipengele vinavyounda fani katika kazi za fasihi. Muundo ni mpangilio wa visa na matukio katika kazi za masimulizi kama vile riwaya, hadithi, tamthiliya na hata ushairi. Katika kazi za semi kama vile methali, muundo hurejelea mpangilio wa sentensi zinazounda semi husika (Mulokozi, 1996). Methali za jamii ya Wasimbiti kama zilivyo methali za jamii mbalimbali duniani zimeundwa kwa pande mbili ambapo upande wa kwanza huwa ni swali na upande wa pili huwa ni majibu ya swali hilo. Hebu tuonebaadhi ya methali kama hizizifuatao:

**Methali:** Nyilandulya yatondaini no nyakolokotwi.

**Tarjama:** Mwendapole alipambana na mwenye nguvu

**Methali:** Hano wasekera omobheru nuryebhora omobheru.

**Tarjama:** Ukicheka kilema, utazaa kilema pia.

Tukitazama methali zote mbili tunaona kuwa zimeundwa kwa muundo wenye pande mbili za sentensi zenye swali na jibu. Muundo huu husaidia wasomaji kuelewa kuwa kama kitu fulani kikifanyika au kisipofanyika basi matokeo yake yanaweza kuwa ni nini? Muundo wa namna hii ni mzuri hata katika kutoa msisitizo juu ya jambo ambalo linaelezwa katika methali iliyotajwa. Hata kwa watoto wadogo ni rahisi sana kukariri methali kutokana na muundo wake ulivyo. Hii husaidia watoto kupata mafundisho yenye hekima na busara yaliyopo ndani ya methali tangu wakiwa watoto. Tunayasema haya kwa sababu muundo wa aina hii huwafanya watoto

kupenda kusema methali na kutajiana baina yao wanapokuwa shuleni au hata nyumbani katika michezo yao.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kwa namna ambayo imesaidia kujibu maswali ya utafiti. Data za utafiti zilichambuliwa kwa kuzingatia madhumuni mahususi matatu ambayo yalikuwa ni kubainisha dhima za methali za jamii ya Wasimbiti, kuelezea uhalisia wa dhima za methali hizo kwa jamii ya leo na kisha kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga mbinu za kisanaa za methali za Kisimbiti. Data za utafiti zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia za Sosholojia na Simiotiki. Kuhusu dhumuni mahususi la kwanza tumebainisha kuwa methali za Wasimbiti zina dhima za kuhimiza wanajamii kuepuka tamaa na kuwa na subira, kuelimisha jamii juu ya masuala yahusuyo maisha, kuhamasisha wanajamii kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, kuwahamasisha wanajamii kuwa na umoja na mshikamano baina yao na umuhimu wa malezi bora kwa jamii. Dhima hizi za methali za jamii ya Wasimbiti zinaonekana kuwa bado zina uhalisia kwa jamii ya leo kwani dhima hizo ni muhimu katika kuiletea jamii hiyo maendeleo. Dhima za methali za jamii ya Wasimbiti zimejengwa kwa kutumia mbinu za kisanaa za lugha ya mafumbo, takriri, taswira na muundo. Sura inayofuata inatoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# 5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho katika tasinifu hii ambayo inatoa hitimisho, muhtasari na mapendekezo kwa ajili ya utafiti zaidi. Sura hii inatoa picha kamili ya kile ambacho kimewasilishwa na kuchambuliwa katika tasinifu hii. Ufuatao ni muhtasari wa tasinifu nzima.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo yote kwa pamoja yamefanyiwa kazi katika tasinifu hii. Madhumuni hayo mahususi yalikuwa ni kubainisha dhima za methali za jamii ya Wasimbiti wa wilaya ya Rorya mkoani Mara, kuelezea uhalisia wa dhima za methali za jamii ya Wasimbiti kwa jamii ya leo na mwisho, kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhima za methali za jamii ya Wasimbiti wa wilaya ya Rorya mkoani Mara. Muhtasari wa kila lengo mahususi unatolewa hapa chini kama ifuatavyo.

### 5.2.1 Dhima ya Methali za Jamii ya Wasimbiti na Uhalisia Wake

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa methali za jamii ya Wasimbiti zina dhima nyingi na muhimu kwa maisha ya jamii hiyo. Hata hivyo katika utafiti huu hatukueleza dhima zote bali tumechunguza dhima 5 tu. Dhima hizo za methali za Wasimbiti ni kuhamasisha jamii kuacha tamaa na kuwa na subira, kuelimisha jamii katika mambo yahusuyo maisha, kuhamasisha jamii kufanya kazi kwa juhudi na

maarifa, kuhimiza umoja na mshikamano katika jamii na kuhimiza malezi bora kwa jamii. Kimsingi, dhima hizi za methali za jamii ya Wasimbiti ni muhimu sana katika kujenga jamii yenye maadili kutoka kizazi kimoja na kingine. Ikiwa kila mwanajamii atazienzi na kuzitumia methali hizi katika kuwafundisha, watoto, vijana na hata watu wazima kuhusu namna ya kuishi maisha bora ni dhahiri kwamba maisha ya jamii hiyo yatakuwa mazuri na mfano wa kuigwa. Methali za jamii ya Kisimbiti zinawataka wanajamii kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kujiletea maendeleo. Methali zinaitaka jamii kuepuka tamaa na kuwa na subira ili waweze kupata maisha mazuri. Methali hizi zinaendana na kauli mbiu ya serikali ya awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosisitiza juu ya kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kwa kusema, 'Hapa ni kazi tu."

Methali za jamii ya Wasimbiti, pia zinazungumzia juu ya suala la malezi ya watoto kuwa ni la jamii nzima na si la mzazi peke yake. Mtoto anayepata malezi kutoka kwa jamii nzima huwa na maadili kuliko mtoto anayefunzwa na wazazi peke yao. Si mara zote mtoto huwa karibu na wazazi lakini huwa na jamii mara zote. Jamii inaaswa kupitia methali za jamii ya wasimbiti kutodhani kwamba kumlea mtoto ni jukumu la mzazi peke yake. Mtoto ni mali ya jamii na anapofanya uhalifu kutokana na kukosa malezi bora hachagui mtu wa kufanyia uhalifu bai ni yeyote tu katika jamii anaweza kufanyiwa uhalifu. Kwa upande wa pili pia, mtoto akipatiwa malezi mazuri na baadae akawa kiongozi, huwa ni kiongozi wa jamii nzima na si wazazi wake tu. Kwa jumla tunaweza kusema kwamba methali za jamii ya Wasimbiti zina uhalisia katika maisha ya jamii ya leo na kazi hii itakuwa ni moja kati ya njia za kufundisha jamii juu ya ukweli huu.

### 5.2.2 Mbinu za Kisanaa katika Methali za Kisimbiti

Methali za jamii ya Kisimbiti zina utajiri mkubwa wa matumizi ya mbinu za kisanaa ambazo zinazifanya methali hizo kuwasilisha dhima zake kwa jamii iliyokusudiwa. Mbinu hizo za kisanaa ni pamoja na matumizi ya lugha ya mafumbo, takriri, matumizi ya taswira na muundo. Mbinu hizi kwa pamoja tumeona kuwa zimekuwa na dhima ya kutoa msisitizo juu ya dhima za methali za Wasimbiti kwa jamii yake. Kwa mfano, karibu methali nyingi za Wasimbiti zimeonekana kuwa na matumizi ya lugha ya mafumbo. Wakati mwingine methali inaweza kuwa imejengwa kwa kutumia lugha ya kawaida lakini ndani mwake mna fumbo ambalo ndilo linaloelezwa. Ipo methali moja ya Kisimbiti inayoeleza kuwa, "mwendapole alimshinda mwenye nguvu." Hii ni methali yenye lugha ya kawaida kabisa lakini ndani yake mna fumbo. Fumbo lenyewe ni kuwa mtu yeyote anayetaka mafanikio katika maisha ni lazima afanye mambo yake taratibu akiwa na mipango madhubuti ya kumwezesha kufanikiwa. Si jambo rahisi kwa mtu yeyote yule kupata maendeleo kwa kukurupuka bali kutulia na kufanya kazi kwa makini.

## 5.3 Hitimisho

Methali za jamii ya Wasimbiti zimeonekana kuwa zina dhima nyingi ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Dhima hizo pia zimeonekana kujitokeza katika methali za jamii mbalimbali za duniani, Afrika na Tanzania. Mathalani dhima za methali za jamii ya Wasimbiti ni sawa na zile za methali za Uingereza, Darfur, Iraq, Sudan, Kenya, Malawi na Jordan. Haya yamejibainisha katika sura ya pili tulipofanya mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sambamba na hilo, methali nyingi za jamii ya Wasimbiti zina dhima

zinazofanana na methali za Kiswahili na kuthibitisha ile nadharia kwamba, wabantu ni wamoja na kinachowatoutisha ni maeneo yao wanayoishi.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti kama huu wetu unaweza kufanywa katika methali za makabila mengine ya Tanzania na Afrika kwa jumla ili kuweza kupata uelewa mpana zaidi.

Pia, utafiti kama huu unaweza kufanywa kwa lengo la kulinganisha na kulinganua dhima ya methali za kabila mojawapo la Tanzania na methali za kabila jingine la nchi yoyote ile ya Kiafrika au hata nje ya mipaka ya Afrika.

**MAREJELEO**


Ahmed, S. (2005). *Educational and Social Values Expressed by Proverbs in Two Cultures: Knowlegde and Use of Proverbs in Sudan and England*, Berlin.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Bathes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*, Berkely: University of Califonia Press.

Bwanamaya, B. J. (2004), "Uhusiano Kati ya Methali na Mabadiliko Katika Jamii." Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Chacha, P. E. (1999). Endangered African Proverbs Collections: Kurya (Kenya, Tanzania) Proverbs, Musoma: Contribution of The African Proverbs Project.

Creswell, J. W. (2000). *Research Design: Qualitative and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Cross, S. (2011). *Sociological Theory and Analysis*, London: University of London.

Eco, U. (1976). *A Theory of Semiotics*, Bloomington: Indiana University Press.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*, London: Clarendon Press.

Hussein, N. (2000). *Women in Popular Proverbs in Jordan and Palestine: A Psychological Study of Women Status and Relatives*: Azmena Publishing House.

Khatibu, M. S. (1986). "Tamathali za Semi za Kiswahili." Katika *Mulika* na 18. Dar es Salaam: TUKI.

Kitogo, S. A. (2002). "The Poets Contribution to Political Development: A case of Saadan Abdul Kandoro", Unpublished *M. A. Thesis* UDSM.

Knappert, J. (1977). *A-Z of African Proverbs*, London: London University Press.

Kothari, C. R. (2008). *Reserch Methodogy: Methods and Techiniques,* New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2000). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi: Pauliness Publications.

Kunemah, A. S. K. (2008). *Misemo na Methali Katika Ushairi,* Dar es Salaam: TATAKI.

Madumulla, J. S. (2005). *Proverb and Saying*: *Theory and Practice,* Dar es Salaam: University Press. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Mark, G. (1995). *Postmodern Semiotics: Material Culture and the Forms of Postmodern Life.* Oxford: Basil Blackwell.

Maitaria, J. N. (1991). "Methali za Kiswahili Kama Chombo cha Mawasiliano: Mtazamo wa Kiisimu Jamii," Tasinifu ya M. A, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Maitaria, J. N. (2010). "Methali Kama Fomula ya Uwasilishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Baadhi ya Mashairi ya Abdilatif Abdalla," Katika *Kioo cha Lugha Juzuu la Nane*, Dar es Salaam: TUKI. Kur. 107-117.

Maitaria, J. N. (2012). "Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali," Tasinifu ya Ph.D, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mbiti, J. S. (1996). *Ethical Concept of God in African Proverbs,* Pretoria: UNISA Press.

Mohammad, S. J. (1988). *The Status and Attitude to Women as Reflected in Arabic Proverbs With Particular Reference to Iraq,* M. A. Dissertation, University of Leeds.

Mohammad, S. J. (1999). *Reflections of Women Emage in Darfur Proverbs*, PhD. Thesisi, Instititute of African and Asian Studies Folklore Department, University of Khartoum.

Mphande, D. K. (2001). *Tonga Proverbs From Malawi*, Lilongwe: Jack Stores.

Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili. Chapa ya Kwanza*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. na Kitogo, S. (2007). *Mithali na Mifano ya Kiswahili- Shaaban Robert*, Dar es Salaam: TUKI.

Mwenerwa, J. (2003). "Methali za Jamii ya Wahaya wa Mkoani Kagera," Tasinifu Ndogo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Nazarova, T. (1996). *Linguistics and Literary Semiotics*, Moscow: Moscow State University Press.

Njogu, K na Chimerah, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.

Nyerere, J. K. (1967). *Ujamaa: The Basis of African Socialism*, Dar es Salaam: Tanganyika Standard.

Oniango, M. C. P. (1978). *The Role of Proverbs and Riddles in Culture of Abaluyia*, Nairobi: EALB.

Robson, C. (2007). *How to do a Research Project: A Guide for Undergraduate Students*, Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Scott, J. (1995). *Sociological Theory: Contemporary Debate*, Cheltenham: Edward Elgar.

Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA.

Sengo, T. S. Y. M. (2012). *Hisiya Zetu*, Dar es Salaam: TATAKI.

Senkoro, F. E. M. K. (2006). "Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano Baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi," Katika *Kioo cha Lugha Juzuu Na 4*, Dar es Salaam: TUKI.

Senzighe, R. (2004). "Usawiri wa Mwanamke Katika Methali za Wapare," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Skeggs, B. (1997). *Formation of Class and Gender*, London: Routledge.

Swingewood, A.A. (2000). *A Short History of Sociological Thought*, Houndsmills: Palgrave.

Turner, B. (1999). *Classical Sociology*, London: Sage.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Webster, F. (2006). *Theories of the Information Society*: London: Routledge.

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) Thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.

# KIAMBATANISHO

**Muongozo wa Usaili kwa Wazee Walioteuliwa**

**A: Utangulizi**

Mimi ninaitwa **Angela Ghati Sylvester** mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili (M.A) katika Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafanya Utafiti wenye anuani isemayo **Kuchunguza Dhima ya Methali za Wasimbiti wa Rorya mkoani Mara**. Ili niweze kupata data za kuweza kukamilisha utafiti huu nimeandaa muongozo huu ambao ndani yake kuna maswali yaliyolengwa kwako na ninaomba nikufanyie usaili.

**B: Taarifa Binafsi za Msailiwa**

Jina………………………………

Elimu…………………………….

Umri……………………………..

Kazi……………………………...

**C: Maswali**

1. Naomba unitajie methali za Kisimbiti unazozifahamu.
2. Methali za Kisimbiti zinatumikaje?
3. Ni zipi dhima za methali za Wasimbiti?
4. Kwa nini methali za Wasimbiti hazisikiki sana hata huku Usimbitini?
5. Unadhani nini kifanyike ili methali za Wasimbiti ziweze kudumu kwa miaka mingi zaidi?

**Asante kwa Kunipatia Muda Wako**